# Nipashe

Alhamisi Mei 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580237

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




Ndugai ashtakiwa rasmi Korti Kuu kisa ubunge wa Mwambe

UKURASA 2



ama

ALHAMISI MEI 21, 2020

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

Dawasa na jumuiya za maji katika ubia kukabili corona

Ukurasa 13

Hofu ongezeko mimba kwa wanafunzi likizo ya corona

Ukurasa 14

Ijue shida ya utapiamlo na undani wake

AFYA

DC: Tutawapima wanafunzi wote baada likizo ya corona

Na Yasmine Protace,

MKURANGA

NI takriban miezi mitatu, tangu ugonjwa wa corona kuingia nchini. Serikali baada ya kuona mambo sivyo, iliagiza kufungwa kwa shule na vyuo, ni kuwabakisha majumbani wanafunzi, kuwaepusha wasipate maambukizo ya ugonjwa huo.

Kukaa nyumbani ni moja ya jitihada za kuwapunguzia wanafunzi wasirundikane katika madarasa, hosteli au bwenini, iwe vyuoni au shuleni.

Katika kuepuka ugonjwa huo, kikubwa kinaelezwa ni kukwepa mikusanyiko, hivyo wanafunzi wakatakiwa kutoendelea na masomo kutokana na mikusanyiko.

Pamoja na katazo hilo, bado kuna baadhi ya maeneo watoto wadogo ambao ni wanafunzi, bado wanazurura ikiwamo katika baadhi ya masoko na vituo vya daladala, wakiendelea na biashara ndogo.

Siku chache zilizopita, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mkuranga, alieleza kusikitishwa na baadhi ya wazazi wanaowaruhusu watoto wao kufanya biashara ndogo katika maeneo mbalimbali ya wilaya, badala ya kutulia nyumbani.

"Kupitia viongozi wetu, tunatakiwa maagizo tuyatii. Watoto wakae nyumbani, wasijiingize katika makundi, pia hata biashara wanazofanya sio sahihi," anasema.

Anaongeza kutokana na ukweli kwamba baadhi yao wanaishia kuzurura mitaani, wanatarajia shule zitakapofunguliwa; msingi na sekondari, watawapima ujauzito.

Pia, Sanga anatoa agizo kwa watendaji wa kata zote wilaya kwake, kwamba waendelee kutoa elimu ya afya na uzazi kwa wazazi na walezi wa wanafunzi hao wa shule, ikilenga mahsusi kuwaepusha na mimba zisizotarajiwa hasa kipindi hiki cha mapumziko ya kupisha janga la corona.

Anaeleza kusikitishwa na baadhi ya wazazi wanaokaidi agizo la kiserikali, ambalo linawasaidia watoto kubaki nyumbani na wakati huohuo, wakijiepusha na vitendo vitakavyoathiri elimu yao.

"Watoto wakae nyumbani, wasijiingize katika makundi, pia hata biashara wanazofanya sio sahihi."

Wanafunzi wa eneo la Vikindu, Mkuranga katika moja ya matukio ya ugeni uliowahusu. PICHA: MTANDAO.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga. PICHA: YASMINE PROTACE

shule zitakapofunguliwa.

Sanga anaitaka jamii iendelee kuchukua hatua kuhusu kujikinga na ugonjwa huo, serikali ikiendelea kuwaunga mkono kwa kuielimisha jamii namna ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Anataja msaada mwingine ni vitakasa mikono vilivyopo katika maeneo mbalimbali yenye mwingiliano wa watu wanakofika kupata mahitaji hasa ya lazima, kama vile hospitali na sokoni.

Pia, ana rai anayowaendelezea wananchi kuendelea kuvaa barakoa, huku madiwani waendelee kuwahamasisha kuchukua tahadhari zinazohusu ugonjwa huo.

Sanga anasema, kuibuka corona isiwe kigezo cha watu kushindwa kuwahudumia wananchi kwa kukaa majumbani, bali kinachotakiwa ni kutoogopa ugonjwa, huduma ziendelee zinavyokusudiwa.

X- RAY YATUA

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Juma Abeid, anazungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani, kwamba kuna hatua waliopiga kwa serikali kuu kuwapatia huduma za X-ray katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga.

Mwenyekiti Abeid, anasema kabla ya msaada huo uliotolewa na Rais Dk. John Magufuli, na wagonjwa walienda kupata huduma hiyo nje ya wilaya na hasa mkoa jirani, kwenye Jiji la Dar es Salaam.

Mwenyekiti huyo kupitia nafasi yake, ni miongoni mwa waliofanikisha zahanati na vituo vya afya kujengwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Wilaya ya Mkuranga.

UKURASA 11

# Magufuli, Kenyatta waingilia kati mipaka

## WAAGIZA mawaziri wakutane haraka kujadili malori kuzuiwa...

*Endelea ukurasa 2*




Wakati wataalamu wa afya wanashauri watu kuwa katika umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu, ili kujikinga na maambukizo ya corona, hali haiko hivyo katika Mtaa wa Congo, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, ambapo jana msongamano wa wananchi na wafanyabiashara ulikuwa mkubwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watafiti wabaini miti 10 inayotibu corona

UKURASA 2

## IDRIS SULTANI MATATANI POLISI

UKURASA 4

## BAA LA CORONA



Mazoezi ya kila siku kwa mwanadamu yana faida katika mwili na akili. Yanapunguza shinikizo la damu, kuuweka uzito wa mwili sawa na kupunguza hatari ya kupata magonjwa ya moyo, kupooza, sukari na saratani. Pia yanaboresha mifupa na misuli. Shirika la Afya Duniani (WHO), linashauri kufanya mazoezi katika kupambana na corona.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


MICHEZO **UTAJIRI WAANZA KUNUKIA YANGA** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Magufuli, Kenyatta waagiza mawaziri

**Na Mwandishi Maalum**

MARAIS John Magufuli wa Tanzania na Uhuru Kenyatta wa Kenya, wamewaagiza mawaziri wanaohusika na uchukuzi na wakuu wa mikoa iliyoko katika pande zote za mpaka wa Tanzania na Kenya, kukutana na kutatua mgogoro uliosababisha kuzuiwa kwa malori ya mizigo kuvuka mpaka huo.

Rais Magufuli alisema hayo jana, alipokuwa akiwasalimu wananchi wa Singida akiwa safarini kutoka Chato mkoani Geita kwenda makao makuu ya nchi jijini Dodoma.

Siku chache zilizopita umeibuka mgogoro katika vituo vya mpaka wa Tanzania na Kenya katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro baada ya malori ya mizigo ya kutoka Tanzania kuzuiwa kuingia Kenya kwa madai ya madereva wanaopimwa kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Rais Magufuli alibainisha kwamba, Rais Kenyatta alimpigia simu juzi na jana, na katika mazungumzo yao, amempa pole kutokana na msiba wa dada yake na pia wamekubaliana kuwa viongozi wa pande zote mbili wanapaswa kukutana na kuutatua mgogoro huo haraka iwezekanavyo ili Watanzania na Wakenya waendelee kufanya biashara zao kama kawaida.

Alisema kwamba kuzuiwa kwa malori ya Tanzania yanayokwenda Kenya ama kuzuiwa kwa malori ya Kenya kuja Tanzania hakukubaliki.

"Haiwezekani madereva wetu wote wawe na corona, haiwezekani magari ya Tanzania yakwamishwe kwenda Kenya na magari ya Kenya yakwamishwe kuja Tanzania, tunataka tuutumie mpaka huu kufanya biashara sisi na ndugu zetu Wakenya, tusichonganishwe na corona," Rais Magufuli alisisitiza.

Aliwataka viongozi wa pande zote mbili waweke maslahi ya Tanzania na Kenya mbele, waache kuamua mambo kwa jazba na akaagiza wakuu wa mikoa ya Mara, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, kuhakikisha mazungumzo hayo yanafanyika ndani ya wiki moja.

Rais Magufuli pia aliwapongeza wananchi wa Singida kwa kuchapa kazi na kujenga mkoa wao ambao umepiga hatua kubwa za kimaendeleo na akawataka waendelee kufanya kazi kwa juhudi na maarifa hasa kuzalisha mazao ya chakula.

Baada ya kusikiliza kero za wananchi, Rais Magufuli alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, kushughulikia haraka mgogoro wa ardhi kati ya familia ya Mzee Masoud na wamiliki wa Sekondari ya Al-Azhary na pia akaagiza vyama vya ushirika vinavyonunua mazao ya wakulima, kuhakikisha vinawalipa fedha zao badala ya kuwakopa.

Kabla ya kufika Singida, Rais Magufuli alikutana na wananchi wa Nzega mkoani Tabora na kuwapongeza kwa kupata maji kupitia mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria ambao kwa sasa upo katika hatua ya majaribio, na akaahidi kuwa serikali itaendelea kushughulikia tatizo la maji katika mkoa huo.

Rais Magufuli alisisitiza Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona (Covid-19), lakini wasikubali kujazwa hofu kiasi cha kuathiri maisha yao na kwamba hiyo ndiyo sababu serikali iliamua kutowafungia wananchi majumbani (lockdown) wala kufunga mipaka.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Misitu Tanzania (TAFORI), Revocatus Mushumbusi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la uhifadhi wa misitu, mkoani Shinyanga jana, kuhusu taasisi hiyo kubaini miti 10 yenye uwezo wa kutibu dalili za awali za mtu mwenye maambukizo ya virusi vya corona. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watafiti wabaini miti 10 inayotibu corona

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TAASISI ya Utafiti wa Misitu Tanzania (Tafori), imebaini miti 10 ambayo ina uwezo wa kutibu dalili za awali za mtu ameambukizwa virusi vya corona.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Revocatus Mushumbusi, aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake ya siku moja mkoani Shinyanga kwenye eneo la uhifadhi wa misitu.

Alisema wamebaini miti 10 ambayo ina uwezo wa kutibu dalili za awali za mtu mwenye maambukizo ya virusi hivyo vilivyotikisa dunia tangu vilipogungulika Desemba mwaka jana Wuhan, China.

Mushumbusi alisema miti ya asili ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na janga hilo kwa ama kujifukiza au kunywa maji yake yaliyochanganywa na mizizi ambayo inatibu dalili za awali, ikiwamo homa kali, kikohozi, mafua, kichwa, kifua kubana na kushindwa kupumua.

"Wakati dunia nzima inapambana na ugonjwa wa corona ambao bado haujapata dawa wala chanjo, na kinachotibika ni dalili zake, Taasisi ya Utafiti wa Misitu tunaamini kuwa kupitia miti hii 10 ya asili ambayo imekuwa ikitibu dalili za magonjwa kama hayo ya corona, wananchi wakiitumia ipasavyo watakuwa salama.

"Miti hii 10 ni Mlungulungu, Nengo Nengo, Mwatya, Mlundalunda, Mfutwambula, Ningiwe, Mgada, Mondo, Msana, Mlungulungu, na Mzima, ambapo mizizi na majani yake, yamekuwa yakitibu magonjwa mbalimbali ambayo yana dalili zote za awali za mtu mwenye maambukizo ya virusi vya corona," alisema.

Alitaja baadhi ya magonjwa ambayo yanatibika kwa kutumia miti hiyo ya asili kuwa ni homa kali, kikohozi, mafua, kichwa, homa ya mapafu, matatizo ya tumbo, kifua, ganzi, malaria, athma, kuharisha, upungufu wa damu, ugumba, kibofu cha mkojo, vidonda vya koo na kushindwa kupumua.

## Ndugai afunguliwa kesi Mahakama Kuu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

SHIRIKA la Uraia na Msaada wa Sheria (Cilao), limefungua kesi namba sita ya mwaka 2020, Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, kumshtaki Spika wa Bunge, Job Ndugai kwa kumruhusu Cecil Mwambe, kuendelea na shughuli za Bunge ilhali amepoteza sifa za ubunge.

Mbali na Ndugai, pia limemshtaki Mwanasheria Mkuu wa Serikali na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ndanda, Mwambe.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha, Mkurugenzi Mtendaji wa Cilao, Odero Odero, alisema shirika hilo limefungua kesi hiyo, kuiomba Mahakama Kuu kutoa tafsiri kuhusu kitendo cha Spika Ndugai kumrejesha bungeni Mwambe wakati alijiuzulu nafasi yake ya ubunge na uanachama wa Chadema na kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hata hivyo, alisema kabla ya kufungua kesi hiyo, shirika hilo lilikusanya maoni ya Watanzania 3,000, waliopinga kitendo cha Spika Ndugai kumrejesha bungeni Mwambe, hivyo limefungua kesi kwa niaba ya watu wote wanaopenda utawala wa sheria nchini.

Alisema sababu ya kufungua kesi hiyo, Ibara ya 26(1) ya Katiba ya nchi ya mwaka 1977, inatoa wajibu wa kila raia kuitii na sheria zake.

Vile vile, alisema Spika wa Bunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Cecil Mwambe wote kwa pamoja wana wajibu wa kutii katiba kwa kuzingatia Ibara ya 71(f) na kifungu namba 6c(3) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, sura ya 288 toleo la mwaka 2002.

Alisema, kwa mujibu wa Ibara ya 71(1)(f) ya Katiba na kifungu namba 6c(2) na 6c(3) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, sura ya 288 toleo la mwaka 2002, mbunge atakoma kuwa mbunge endapo atajiuzulu nafasi yake ya ubunge na kuhamia chama kingine kama ambavyo Cecil Mwambe alivyojiuzulu.

Alisema kwa uzoefu wa uendeshaji wa shughuli za kibunge, utaratibu wa kikatiba ulishawahi kutolewa ufafanuzi na Spika kwenye kesi ya Abdallah Mtulia, Mwita Waitara, Dk. Godwin Mollel, Katani Ahmad Katani na wengine, ulidhihirisha wazi kwamba mbunge akitangaza kujiuzulu na kuhamia chama kingine basi atakuwa amepoteza sifa ya kuwa mbunge.

Odero alisema shirika hilo, linaamini Mahakama Kuu itatenda haki kwa kutoa tafsiri sahihi ya Katiba na Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Shirika la Cilao, linapenda kuwashukuru Watanzania wote waliotoa maoni yao kuhusu kupinga kitendo cha Spika Job Ndugai, kumrejesha bungeni Cecil Mwambe," alisema Odero.

Katika kesi hiyo, Cilao inatetewa na Wakili John Seka na Mahakama Kuu itapanga tarehe ya kusikiliza kesi hiyo wiki ijayo.

Hivi karibuni, Ndugai alitangaza bungeni kuwa hajaridhishwa na barua iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, kuhusu kumzuia Mwambe kushiriki shughuli za Bunge na kulipwa stahiki zake za ubunge.

## HABARI KITAIFA



Mfanyabiashara wa miguu ya ng'ombe, akiiandaa wakati akisubiri wateja nje ya machinjio ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam juzi. Wateja wakubwa wa bidhaa hiyo ni wafanyabiashara wa supu ya kongoro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kinachojiri mpakani ni hujuma utalii -RC

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, amesema ofisi yake imebaini mbinu chafu zinazofanywa kwa lengo la kuharibu biashara ya utalii nchini, hususani katika jiji hilo la kiutalii.

Mrisho Gambo amesema moja ya mbinu walizobaini ni madereva 19 wa malori kutoka Tanzania, ambao walipimwa Kenya na kuonekana wana maambukizo ya virusi vya corona, lakini walipopimwa nchini majibu yakaonyesha hawana maambukizo.

Taarifa iliyotolewa jana jijini hapa kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Mkoa huyo, ilisema ofisi yake imejiridhisha kuwa hizo ni mbinu chafu za majirani kutaka kuua soko la utalii katika Mkoa wa Arusha na Tanzania kwa ujumla.

Katika taarifa yake hiyo, Gambo alisema waliamua kuchukua upya baadhi ya sampuli za madereva 19 raia wa Tanzania, walioopimwa katika Mpaka wa Namanga upande wa Kenya na kuzipeleka Maabara Kuu ya Taifa iliyoko jijini Dar es Salaam, ambako majibu yalionyesha kuwa madereva hao hawakuwa na maambukizo ya ugonjwa huo.

"Hizi ni mbinu chafu za nchi jirani za kutaka kuua soko la utalii katika Mkoa wetu wa Arusha na Tanzania kwa ujumla, kwa sababu baada ya vipimo vyao kudai kuwa madereva wetu 19 wana maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19, tulijiridhisha.

"Tulichukua sampuli za madereva hao na kuzipeleka kwenye Maabara Kuu ya Taifa jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupimwa na majibu yalitoka kuwa madereva hao walikuwa 'negative' (hawana maambukizo)," Gambo alisema katika taarifa yake hiyo.

Kwa mujibu wa Gambo, kutokana na ongezeko la maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 kupitia mipakani, Mkoa wa Arusha umeanzisha utaratibu wa kuchukua sampuli za madereva wa malori wanaopita Mpaka wa Namanga kutoka Kenya tangu Mei 14 mwaka huu.

Alibainisha kuwa sampuli zote zilizochukuliwa na wataalamu wa afya kuanzia siku hiyo hadi Mei 18 mwaka huu zimepelekwa Maabara Kuu ya Taifa jijini Dar es Salaam na kupata majibu ya vipimo husika.

"Utaratibu wa kuchukua sampuli ili kupima Covid-19 kwa madereva wa malori wanaotoka Kenya, ulianza kutumika rasmi Mei 14 mwaka huu na majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

"Madereva 44 kutoka Kenya waliochukuliwa sampuli Mei 14, mwaka huu na majibu yalitoka Mei 16, mwaka huu, madera 11 raia wa Kenya walikuwa na maambukizo ya covid-19, dereva mmoja kutoka Uganda na madereva wawili ambao majina ya nchi yao yanahifadhiwa na madereva 30 hawakuwa na maambukizo.

"Mei 16 mwaka huu, madereva 23 kutoka Kenya walichukuliwa sampuli ambazo pia zilipelekwa Maabara Kuu ya Taifa na majibu yalitoka Mei 19, mwaka huu, ambapo madereva 10 raia wa nchi hiyo walikutwa na maambukizo hayo na madereva 13 hawakuwa na maambukizo."

Gambo pia alisema Mei 18 mwaka huu, madereva 11 kutoka nchi jirani walichukuliwa vipimo na majibu yake yatatangazwa baada ya majibu kupatikana kutoka Maabara Kuu ya Taifa ya jijini Dar es Salaam.

"Tumechukua uamuzi huu ili kuwalinda wananchi wetu dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 kutoka Kenya pamoja na kuimarisha usalama wa afya ya wananchi wetu kama sehemu ya maandalizi ya kupokea watalii msimu msimu utakapoanza mapema mwezi Juni mwaka huu," alisema.

Gambo alisisitiza kuwa kuanzia sasa, madereva wote watakaopimwa na kukutwa na maambukizo ya Covid-19, hawataruhusiwa kuingia nchini wala kwenda Kenya na kwamba Mkoa wa Arusha unaendelea kuchukua tahadhari na kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo kwenye Mpaka wa Namanga.

Kwa takriban wiki mbili sasa, kumekuwa na malalamiko ya madereva wa Tanzania kulazimishwa kupimwa mpakani Namanga na wataalamu wa afya kutoka Kenya na kudaiwa wengi wao wana maambukizo ya virusi vya corona.

# M/Kiti Bavicha ashtakiwa kuchapisha picha za ngono

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), Mkoa wa Kilimanjaro, Lemruce Mchome (30), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na tuhuma za kusambaza nyaraka za ngono ikiwamo picha na video kwa nia ya kuleta ashki za ngono kinyume cha sheria.

Kigogo huyo ambaye ni mkazi wa Kisaranga, Wilaya ya Mwanga, amesomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kuweka, alidai kuwa kati ya Januari Mosi na Aprili 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam mshtakiwa alitenda kosa la kusambaza nyaraka za ngono.

Kweka aliendelea kudai kuwa Mchome alisambaza nyaraka za ngono ikiwamo picha na video za mwanamume kupitia simu yake ya mkononi kwa nia ya kuleta ashki za ngono kitu ambacho ni kinyume cha sheria.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo na upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hata hivyo, Kweka aliiomba mahakama isitoe dhamana kwa mshtakiwa huyo kwa sababu upelelezi unaendelea.

Mchome alidai mashtaka hayo yamemshtua kwa kuwa alikamatwa Mei 11, mwaka huu, lakini amezuiliwa kuonana na ndugu zake pamoja na wanasheria.

Alidai kesi hiyo sio ya kwanza kwa mahakama hiyo kwa kuwa zipo ambazo zilitolewa dhamana huku upelelezi ukiendelea.

Akijibu hoja hiyo, Kweka alidai huo ni mkakati wao wa kuendelea na upelelezi.

Hakimu Mwaikambo alisema uamuzi wa mabishano ya pande zote mbili kuhusu dhamana itatolewa Juni 2, mwaka huu, mshtakiwa arudishwe mahabusu.





**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni Shoponline Tanzania **www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**



Katibu Mwenezi wa Chama cha Tanzania Labor Party (TLP), Geoffrey Stephen, akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha jana, kuhusu chama kujiandaa kusimamisha wagombea nchi mzima katika uchaguzi mkuu ujao. Kulia ni Katibu wa TLP Mkoa wa Arusha, Kinanzaro Manga. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Serikali yapata dawa ya kunufaika na bahari kuu

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SERIKALI imekuja na mkakati wa kudumu wa kuiwezesha Tanzania kunufaika na rasilimali zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, kwa kufuta Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya Mwaka 1998 na kutunga sheria mpya.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema sheria hiyo ni mwendelezo wa jitihada za serikali kuweka mazingira bora ya uwekezaji na usimamizi katika uvuvi wa Bahari Kuu.

Waziri Mpina alisema mbali na kutungwa kwa sheria hiyo mpya, Serikali ya Jamhuri wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zinatekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo kufufua mashirika ya uvuvi yaani TAFICO na ZAFICO, akibainisha kuwa ununuzi wa meli kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu uko katika hatua mbalimbali huku ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ukiwa katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu.

Alitaja sababu za kutungwa kwa sheria hiyo mpya kuwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vilivyoonekana katika sheria ya zamani ikiwamo kutokuzingatia masuala muhimu ya kusimamia meli za uvuvi zinazopeperusha bendera ya Tanzania nje ya mipaka ya bahari ya Tanzania.

Pia, sheria hiyo ya zamani kutozingatia suala la uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi (conservation and management measures), udhibiti wa uvuvi haramu (Illegal Unreported and unregulated fishing - IUU), udhibiti wa bandari (port state measures) pamoja na uwezo wa mawaziri wenye dhamana kuingia mikataba ya uvuvi (bilateral fishing agreements).

Kutowapo masharti ya ukusanyaji na ubadilishanaji wa taarifa za uvuvi na mavuno ya samaki na uhifadhi wa mazingira ya EEZ na vivutio (incentives) kwa wavuvi na wawekezaji wa Kitanzania.

Waziri Mpina alisema matarajio ya serikali kwa kutungwa kwa sheria hiyo mpya ni pamoja na kuchochea uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na rasilimali za uvuvi wa Bahari Kuu.

Pia, sheria hiyo mpya itawezesha kuimarika kwa uhusiano wa kikanda na kimataifa kutokana na kupungua kwa matokeo ya uvuvi haramu na kuimarika udhibiti na ufuatiliaji wa meli za uvuvi zinazopeperusha bendera ya Tanzania zinapovua nje ya mipaka ya nchi katika Bahari Kuu (High Seas) na EEZ za nchi nyingine.

"Matokeo mengine ni kuimarika kwa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za uvuvi na mavuno ya samaki utakaounganisha taarifa za maji ya ndani, maji ya kitaifa na eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari na kupelekea kuongezeka kwa uwekezaji kwenye sekta ya uvuvi," alifafanua.

Waziri Mpina pia alisema sheria mpya itawezesha kuimarika kwa viwango vya utekelezaji wa taratibu na miongozo ya kikanda na kupungua kwa makosa yatokanayo na ukiukwaji wa sheria nchini.

Alisema madhara yaliyojitokeza kwenye sheria iliyofutwa ya mwaka 1998 ni pamoja na kukosekana kwa utaratibu wa usimamizi wa meli za uvuvi zinazopeperusha bendera ya Tanzania, hali iliyosababisha kukosekana ufuatiliaji wa karibu na kusababisha meli zinazovua nje ya Tanzania kuhusishwa na uvuvi haramu ikiwamo Meli ya Haleluya inayopeperusha bendera ya Tanzania nchini Colombia na kuhusishwa na uvuvi wa papa kinyume cha sheria.

"Katika mwaka 2020/2021, serikali itanunua meli tatu za uvuvi na kuanza uvuvi wa Bahari Kuu na maeneo mengine; kujenga na kuendesha viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi; kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Tafico itakayojumuisha gati la kuegeshea meli za uvuvi, kusimika mitambo ya barafu, maghala ya baridi pamoja na kuiwezesha Tafico kuanza miradi ya ukuzaji viumbe maji.

"Pia, katika juhudi za kuwezesha ujenzi wa bandari ya uvuvi, mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Tanzania na Korea ya Kusini kwa ajili ya kupata ufadhili wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo litakalopendekezwa katika mwaka 2020/2021. Serikali itakamilisha upembuzi wa kina na kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo litakalochaguliwa.

"Uwapo wa Bandari ya Uvuvi utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania na Bahari Kuu kutia nanga, kushusha mazao ya uvuvi na kupata huduma mbalimbali zikiwamo mafuta na chakula," alisema.

Wakati huo, Bunge limetaka kuwapo na udhibiti wa uvuvi wa papa katika bahari kuu, kutokana na watu kutumia mapezi yake kwa ajili ya supu na tiba asili.

Pia, limependekeza kuwa mtu yeyote atakayekutwa na mapezi ya papa bila ya kuwa na mwili atakuwa ametenda kosa kisheria.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitoa mapendekezo hayo jana bungeni, ilipowasilisha maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Ritta Kabati, akisoma maoni hayo, alisema kuna haja kuwekwa kwa masharti ya udhibiti wa samaki aina ya papa katika sheria hiyo.

Kabati alisema muswada huo hauna masharti kuhusiana na samaki hao na kwamba wamekuwa wakivuliwa sana duniani na kukatwa mapezi kwa ajili ya supu na tiba za asili hususani kwa soko la China na sehemu yote ya mwili iliobaki hutupwa baharini.

"Kwa mujibu wa kanuni za uvuvi wa bahari kuu zinazotumika hivi sasa, zinabainisha kuwa mtu yeyote atakayekutwa na mapezi ya papa bila kuwa na mwili atakuwa ametenda kosa kisheria," alisema Kabati na kuongeza:

"Kanuni hizo zinafafanua zaidi kuwa iwapo mtuhumiwa atakutwa na hatia adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi bilioni moja au kifungo cha miaka 10 ishirini au adhabu zote kwa pamoja."

Alisema utaratibu wa mtu anayekutwa na mapezi ya samaki aina ya papa kuwa ni kosa la jinai unatumika katika nchi nyingi duniani kwa sababu mbalimbali.

Alisema miongoni mwa sababu hizo ni utunzaji wa mazingira ya baharini, kulinda baadhi ya aina za papa ambao wanatajwa kuwa hatarini kutoweka.

Alisema watetezi wa haki za viumbe hao wanaeleza kuwa ni ukatili kumkata papa mapezi na kumtupa baharini akiwa hana uwezo wa kuogelea.

"Kwa misingi hiyo, kamati inapendekeza kuwa, ni vyema masharti ya kuwalinda samaki aina ya papa yakazingatiwa katika muswada huu," alisema.

# Idris Sultan mikononi mwa polisi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi linamshikilia mchekeshaji Idris Sultan, baada ya kukamatwa tena juzi jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Edward Bukombe, aliliambia Nipashe jana kuwa, Idris alikamatwa na kufikishwa Kituo cha Polisi Oysterbay ingawa kwa wakati huo (jana jioni) alikuwa ameshaondolewa na kupelekwa Makao Makuu ya jeshi hilo kwa mahojiano.

"Aliletwa hapa ingawa kwa sasa hayupo hapa, amepelekwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kwa mahojiano, wao ndiyo wanaweza kusema chochote," alisema.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alipoulizwa kuhusu suala hilo, alisema kwa wakati huo alikuwa jijini Dodoma na kuahidi kufuatilia na alipotafutwa baadaye jioni, simu yake ilikuwa ikiita bila kupokewa.

Mwaka 2014, Idris alishinda tuzo za Big Brother Africa na mwezi Machi mwaka huu alifikishwa katika Mahakama ya Kisutu kwa kuweka maudhui mtandaoni bila leseni.

# Mama matatani tuhuma za kutupa mwanawe kichakani

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamsaka mwanamke ambaye hajafahamika jina, mkazi wa Mwakitolyo wilayani Shinyanga, kwa madai ya kumtupa mtoto wake mdogo kichakani.

Inadaiwa kuwa alimtupa mtoto huyo mwenye umri wa miaka miwili akiwa ameviringisha Kanga.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira asubuhi, ambapo mtoto huyo aligunduliwa na wananchi akiwa ametupwa vichakani.

Alisema baada ya wananchi kumgudua mtoto huyo akiwa ametupwa vichakani, walitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi, huku mtoto akikimbizwa kwenye Zahanati ya Mwakitolyo na kupewa huduma ya kwanza, na kwamba hali yake inaendelea vizuri chini ya uangalizi wa karibu.

"Tunamsaka mwanamke mmoja mkazi wa Mwakitolyo kwa kosa la kumtupa mtoto wake wa miaka miwili vichakani, na kumviringisha na kanga kisha kumtelekeza," alisema Magiligimba.

Kamanda anatoa wito kwa wakazi wa eneo hilo kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi hilo ili kufanikisha mwanamke huyo akamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.




Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omari Kumbilamoto (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya corona vyenye thamani ya Sh. milioni 7.9 kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Waendesha Bajaji Mkoa wa Dar es Salaam, Nyaikoma Msabi (kushoto), uliotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kushirikiana na Umoja wa Watanzania waliosoma Australia, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waandishi Pwani wasaidiwa vifaa vya kujikinga corona

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

MDAU wa maendeleo Wilaya ya Kibaha Mjini, Abubakary Alawi, ametoa vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 kwa waandishi wa habari mkoani Pwani.

Alawi alisema ametoa msaada huo ili kuwasaidia waandishi kuendelea kujikinga na corona kutokana na mazingira wanayofanyia kazi.

Akikabidhi msaada huo jana katika ofisi za waandishi wa habari mjini Kibaha kwa niaba ya mdau huyo wa maendeleo, Jeremia Komba alisema, utawasaidia waandishi wanapokuwa kazini katika harakati za kuendelea kuuhabarisha umma.

Aliwasihi waandishi kutumia vizuri vifaa hivyo kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu ili waepuke maambukizo ya ugonjwa huo.

Akishukuru baada ya msaada huo, Katibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Pwani (CRPC), Gustaf Haule, alimshukuru mdau huyo kwa kuwakumbuka waandishi.

Haule alisema, msaada huo utawasaidia waandishi wa habari kutokana na kazi ambazo wanakutana na watu mbalimbali katika shughuli zao.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, amesema hali inaendelea vizuri, lakini tunatakiwa tuendelee kujikinga hadi itakapotangazwa kuwa ugonjwa huu umeisha," alisema Haule.

Pia aliomba wadau wengine kuendelea kujitokeza kusaidia vifaa kinga kwa kundi hilo la waandishi kwa kuwa ni mahitaji yao ya kila siku katika shughuli zao.

# Wanasiasa waonywa kubeza corona

Na Faustine Feliciane

WANASIASA nchini wametakiwa kuungana na kuacha kutumia nguvu kubwa ya kubeza ugonjwa wa corona kama mtaji wa kufanikisha matakwa yao ya kisiasa.

Ushauri huo umetolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Siasa na Dini wa Taasisi ya Tanzania Peace Foundation, Dk. Sulle Seif, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini pamoja na kumpongeza Rais John Magufuli kwa kuonyesha msimamo wake usioyumba kuhusiana na ugonjwa wa corona.

Seif alisema ni vyema wanasiasa wakaungana na Rais Magufuli na timu yake ili kupambana na janga hilo kinaloikabili dunia kwa sasa.

"Wapo baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitumika kwa makusudi kupotosha ukweli wa jambo hili na kusababisha hofu kwa wananchi kitu ambacho hakiwezi kusaidia kutokomeza ugonjwa huu, Rais wetu ameonyesba msimamo thabiti wa kupambana na ugonjwa huu akiweka mbele maslahi ya taifa na watu wake, tunapaswa kumuunga mkono ipasavyo," alisema.

"Nawaasa wanasiasa wa aina hii waache kupotosha wananchi kwa kuwa wanadai Tanzania haijafuata ushauri na maelekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) na badala yake tushirikiane kujenga nchi," alisema Seif.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Sadiki Godigodi, alisema kauli na misimamo ya Rais Magufuli zimesaidia kuimarisha afya za Watanzania tofauti na ilivyotazamiwa.

Alisema endapo Rais angeamua kuwafungia Watanzania wasifanye shughuli zozote, ingeweza kuchangia maafa zaidi tofauti na ugonjwa wenyewe.

"Katika kipindi hiki Watanzania wengi wametambua kuwa serikali iliyopo madarakani ni ya wanyonge kwa kuwa imetambua adha ambayo tungeipata hasa watu wenye kipato cha chini," alisema Godigodi.

Pia, alisema kwa sasa wanashuhudia mataifa mengi yameanza kutumia mbinu alizozitumia Rais Magufuli katika kupambana ma ugonjwa huo.

"Tunampongeza Rais wetu kwa kuliona jambo hili mapema na kuamua kutowatesa wananchi wake, kikubwa kinachohitajika ni ushirikiano katika jambo hili na kufuata maelekezo ya wataalam huku kila mmoja akiendelea kuchukua tahadhari kama inavyoelekezwa na wataalam," alisema Godigodi.

Alisema hotuba yake aliyoitoa mwishoni mwa wiki Chato mkoani Mwanza imeamsha ari mpya kwa wananchi wengi kuanza kufanyakazi kwa kujituma zaidi tofauti na awali ambapo kuna baadhi ya watu walianza kuwakatisha tamaa.

KUMBUKUMBU



NECHI EPHRAIM LYIMO
(Mtoto wa Mchungaji)

Leo tarehe 21/05/2019 umetimiza mwaka mmoja toka ulipotwaliwa na Bwana wetu Yesu Kristo kwenda katika makao yako ya milele. Maisha yako yamekuwa ni hazina na baraka kwetu. Tutakukumbuka daima hasa kwa mafunzo yako na ucheshi wako hata wakati unapitia vipindi vigumu.

Unakumbukwa sana na **mkeo Jane** na binti yako **Pelesia,** kaka zako, dada zako, mashemeji, watoto wako katika ukoo, ndugu, jamaa na marafiki

"Sisi tunatoka kwa Bwana na Kwake tutarejea.
Jina la Bwana lihimidiwe."

157463

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji kuvumiliana kwenye suala la mipaka

**KUFUNGA** mipaka baina ya nchi jirani kulikofanywa wiki iliyopita kunatajwa kuwa ni jitihada za nchi kudhibiti maambukizo ya corona. Ilianza kwa Kenya kufunga mpaka wake na Tanzania na kukataza raia na wasafiri kutoka Tanzania kuingia ndani ya taifa hilo.

Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta, alitangaza wiki iliyopita kuwa mipaka ya Tanzania na Somalia itafungwa, isipokuwa tu yataruhusiwa magari ya shehena. Ni kutokana na ongezeko la maambukizo ya corona yanayochangiwa na safari za kuvuka mipaka.

Aidha, tuliyasikia maagizo yake yaliyotolewa wiki iliyopita Mei 16 na haikuishia hapo nchini Zambia Rais Edgar Lungu, alitangaza kufunga mipaka kati ya Tanzania na Zambia kwa maelezo kuwa ni kudhibiti kuenea kwa corona kunakosababishwa na mwingiliano wa raia wa nchi jirani kuvuka mipaka.

Ni jambo lililofanyika na viongozi na kwa Kenya ilikuwa ni lazima kwa madereva kupimwa corona na baadhi waliviambia vyombo vya habari vya kimataifa kuwa walilazimishwa kupimwa kwa kutumia kipimo kimoja na kwamba iwapo wana maradhi watarudishwa nyumbani mara moja.

Madereva wa Tanzania waliokwenda Rwanda walifanyiwa pia mambo ambayo hayakupendeza masikioni kwani walivieleza vyombo hivyo kuwa wanapoonekana mitaani, raia waliziba nyuso zao na kuwatuhumu kuwa wanawasambazia corona.

Kwa ujumla hadithi za kufunga mipaka hazikuwapendeza wengi na serikali ililipokea na kulifanyia kazi ndipo Mkuu wa Mkoa wa Tanga akatangaza kufunga mpaka wa Horohoro na kuwa mwanzo wa malalamiko.

Aidha, mkoani Mara na Arusha ilifungwa pia, serikali mikoani humo ikieleza kuwa itahusika na kuzuia malori na wasafiri kutoka Kenya ili kudhibiti usambaaji wa ugonjwa unaoanzia mpakani.

Tumekisikia kilio cha Kenya na kutafakari kile madereva wa Tanzania walichosema na kufuatilia taarifa za usafirishaji katika mataifa mengine nje ya Afrika na kuona kuwa suala la biashara na usafirishaji wa shehena na abiria linahitaji kuridhiana na si kukurupuka ambako mara nyingi huishia kuumizana.

Kwa mataifa ya Afrika Mashariki, Nchi za Jukuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na hata masuala ya kiukanda na mtangamano kwa ujumla tunakumbushana kuwa kila mmoja anamtegemea mwenzake bila kujali kuwa tupo ndani ya mipaka yetu. Ni vyema kutendeana kwa upole, haki na ikibidi kuwasiliana na kuweka taratibu zisizoumiza kwani kukomoana hakusaidia mtu au taifa lolote.

Ikumbukwe kuwa kuwakwamisha madereva wa Tanzania na shehena zao ndani ya Kenya au Rwanda na hata kuwarudisha nyumbani wenye corona au kuwapima na kipimo kimoja cha kutumbukiza pamba puani au kooni ili kupata ute wenye virusi ni jambo linalostahili kuomba radhi.

Tukizungumzia kutumia kipimo kimoja ni kinyume cha haki za binadamu na kama ni kweli ni kuwaambukiza watu magonjwa kwa makusudi. Ndiyo maana tunasema usimtendee mwenzako usilotaka kutendewa naye.

Kutaarifiwa kuwa unaumwa corona rudi kwenu ukatibiwe ni kwenda kinyume na ubinadamu. Suala la shehena kuzuiliwa mpakani haijalishi ni ya kutoka taifa gani. Ni biashara. Kuna muda unaopotea, gharama inayopatikana na mwisho kinachojiri ni hasara.

Kinachotokea mpakani sasa baada ya Tanzania kufunga mpaka ni udhihirisho kuwa mkuki kwa mnyama ni mtamu lakini kwa binadamu ni mchungu.

Tukumbuke mataifa yetu yanategemeana kiuchumi, kibiashara na hata kujikimu. Ni wazi bidhaa za vyakula na mahitaji muhimu ya binadamu yanaweza kutoka upande mmoja wakati vitu vya viwandani vinazalishwa kutoka nyingine. Hivyo viongozi tuheshimiane na kuacha ubabe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni nzuri Kibiti kufanyisha kazi wanaokiuka ya corona



Na Yasmine Protace, KIBITI

**KATIKA** kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona, utekelezaji katika kuipiga vita, kuna hatua za kujikinga. Jamii zimetakiwa kuzifuata, ili kuukwepa ugonjwa huo.

Muhimu na kinachohimizwa ni kuchukuliwa hatua mapema, kwamba ni jambo jema linalomsaidia mtu asiangukie katika tatizo.

Wataalamu kutoka sekta ya afya, wakiwamo viongozi wa ngazi za juu, pia wasanii, wamekuwa wakitoa elimu ya jinsi ya kujilinda kwa maambukizo hayo ya corona.

Mtu anatakiwa ajilinde dhidi ya maradhi hayo na kisha awalinde wengine.

Katika kujilinda mtu asipate, inaelezwa haja ya kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima kuosha mikono kwa maji tiririka na kuvaa barakoa mara zote, ikiwamo kutumia vitakasa mikono.

Ni elimu inayotolewa kupitia kazi za wasanii na kauli za viongozi, kwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Hiyo yote imo katika kuisaidia jamii isipate maambukizi ya ugonjwa huo.

Inaelezwa, ukweli ni kwamba iwapo jamii itazingatia elimu hiyo, haki hiyo itasaidia watu kutopata maambukizo ya ugonjwa huo.

Kama jamii haitatilia maanani maagizo yanayotolewa jinsi ya kujilinda na maambukizo ya corona hali hiyo itafanya watu kupata maambukizo.

Katika kupambana na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, imetangaza hatua zitakazochukuliwa dhidi ya watu watakaokamatwa wakiwa wamekaa makundi vijiweni.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gulam Musini Kifu, katika kikao cha Baraza la Madiwani kutokana na kuwapo ugonjwa wa corona, hivyo kila mtu anatakiwa kuchukua hatua.

Anasema, baadhi ya watu bado hukaa vijiweni, wanaendeleza mikusanyiko ambayo imekatazwa na serikali na kwa sababu za usalama kiafya, jambo ambalo si zuri.

"Kutokana na watu kutosikia makatazo ambayo serikali inatutangazia kila siku katika kujikinga na corona, sasa Kibiti nimeishamwambia OCD (Kamanda wa Polisi wa Wilaya) wakiwakuta vijana vijiweni wawakamate, wawapeleke sokoni, ofisi ya mkurugenzi, kituo cha polisi na hospitali wakafanye usafi, ikifika jioni wawaachie waende makwao," anasema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya, jambo la kuwafanyisha kazi za usafi wanaokaa vijiweni, itasaidia kupunguza mikusanyiko isiyo na faida.

Pia, anawataka madiwani pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya kuwa wanatakiwa kuwahamasisha wananchi uvaaji wa barakoa.

"Mnapoenda kuhamasisha wananchi uvaaji wa barakoa, hakikisheni na nyie mnaenda mkiwa mmevaa," anasema.

**"Kutokana na watu kutosikia makatazo ambayo serikali inatutangazia kila siku katika kujikinga na corona, sasa Kibiti nimeishamwambia OCD (Kamanda wa Polisi wa Wilaya) wakiwakuta vijana vijiweni wawakamate, wawapeleke sokoni, ofisi ya mkurugenzi, kituo cha polisi na hospitali wakafanye usafi, ikifika jioni wawaachie waende makwao," anasema.**

# Mtuhumiwa alivyouawa akijibizana risasi na polisi

**Na Hamida Kamchalla, TANGA**

MTU mmoja anayesadikiwa kuwa jambazi ameuawa na polisi mkoani hapa huku mwingine akijeruhiwa baada ya majibizano ya risasi.

Kamanda wa polisi mkoani hapa, Blasius Chatanda, alisema mtu huyo alikuwa akipanda juu ya ukuta tayari kwa kuvamia nyumba na kuiba akiwa na bunduki aina ya shotgun huku mwenzake akiwa chini kumuwekea ulinzi.

Alisema tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia jana saa tisa katika mtaa wa Mbolea, kata ya Ngamiani kati, ambako majambazi hao walivamia nyumba ya Jamali Mbarouk (60), mfanyabiashara.

Alisema baada ya majambazi hao kuvamia nyumba hiyo askari polisi walikuwa doria na walipowaona waliwazingira na kuanza kupambana na majibizano ya risasi huku jambazi huyo aliyejulikana kwa jina maarufu 'Macho makavu' alipigwa risasi na kufariki papo hapo.

Alisema wakati wanajiandaa kumkabili jambazi mwingine walifanikiwa kumpiga risasi na kumjeruhi, lakini aliokolewa na wenzake waliokuwa nje ya nyumba huyo kwa njia isiyojulikana.

Kamanda alibainisha kuwa majambazi hao kabla hawajafanya tukio hilo, walishafanya mauaji ya mlinzi wa ofisi ya Brac, mtaa wa Usagara na kuvunja ofisi hiyo, na kuiba Sh. 200,000.

Vilevile Chatanda alitoa rai kwa wananchi mkoani hapa na kusema kuwa ili jeshi la polisi liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuwalinda raia na mali zao inawapasa waendelee kushirikiana kwa ukaribu na kutoa taarifa kwa jeshi hilo bila kuhofia.

Alisema yeyote atakayejihusisha na vitendo vya kihalifu hatoweza kudumu kwa kuwa jeshi hilo limejipanga kukabiliana na uhalifu ndani ya mkoani na hata kwenye mipaka yake.

Aliwataka wananchi wawe na amani katika kusherehekea sikukuu huku akiwaasa kutofanya misongamano ili kuendelea kujikinga na maambukizo ya corona.

"Tumeendelea kuimarisha ulinzi hasa pale Horohoro na tunawahakikishia wananchi wafanye kazi zao kwa amani pia katika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu washerehekee kwa amani bila hofu ya kuvamiwa, lakini tusifanye misongamano kwenye kumbi za tarehe," alisisitiza.

"Disko toto marufuku, atakaeleta tamaa ya kufungua kumbi kwa ajili ya kupiga muziki na kuwakusanya watoto tutamshughulikia, tusiwaache watoto watembee peke yao hasa huko kwenye maeneo ya fukwe, mnaweza kuanza kusherehekea vizuri mwisho wake ukawa mbaya," alisema.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, akionyesha bunduki aina ya shotgun, kwa waandishi wa habari, ofisini kwake, jana, baada ya kuikamata mikononi mwa watuhumiwa wa ujambazi pamoja na silaha nyingine. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Polisi yawaita walioibiwa kutambua mali

**Na Francis Godwin, IRINGA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa, limewataka wananchi wa mkoa huo kufika kituo cha polisi cha Iringa mjini kutambua mali zinazosadikika kuwa ni za wizi zilizokamatwa kwenye msako.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, akitoa taarifa jana kwa waandishi wa habari, alisema kuwa mali hizo zimekamatwa katika msako maalum ulioendeshwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema miongoni mwa mali zolizokamatwa ni pamoja na radio,TV, magodoro, Laptop, simu na mali nyingine.

Pia, jeshi hilo limekamata vifaa vya kijadi ambavyo vilikuwa vikitumiwa na wahalifu hao kuvunja na kuiba mali.

Kamanda Bwire alisema Jeshi la Polisi linaendelea na msako wa kuwabaini washukiwa wa uhalifu na kuwashughulikia kwa kuwafikisha mbele ya sheria.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kuwafichua wahalifu katika mitaa yao wanaojihusisha na matukio ya kihalifu.

Wakati huo huo, jeshi hilo limepiga marufuku mikusanyiko na disco wakati wa sherehe za Eid zinazotarajia kufanyika mwishoni mwa wiki.

# Wateja 265 Benki Stanbic wapata ahueni ya madeni

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA athari za kiuchumi zilizosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa (COVID-19) unaosababishwa na virusi vya corona, Benki ya Stanbic Tanzania imetangaza kutoa unafuu wa malipo ya mikopo kwa wateja wake kwa muda wa miezi 3 hadi 6.

Ahueni hiyo ya malipo iliyoanza Aprili ikilenga sekta ya utalii pekee, hivi sasa imeongezwa na kulenga sekta zingine kama usafirishaji, nishati na wafanyabiashara wa kati na wadogo. Hatua hiyo ni sehemu ya mikakati endelevu yenye lengo la kuwawezesha wateja wa benki hiyo kukabiliana na adha za kiuchumi zitokanazo na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Mkuu wa Idara ya Huduma Binafsi na Biashara, Brian Ndadzungira, alisema kuwa benki hiyo inatambua umuhimu wa wateja wao kuendelea kujishughulisha licha ya uwepo wa janga la Covid-19.

"Tunaelewa kwamba shughuli za kibiashara nchini zimeathirika kutokana na hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani katika kupambana na ugonjwa huu. Hivyo tukaamua kuja na suluhisho ambalo litasaidia kupunguza athari za kifedha zinazowakabili wateja wetu," alisema na kuongeza:

"Tunaimani kwamba hatua hii haitasaidia tu wateja wetu wa biashara ndogo na kati kuweza kumudu ulipaji wa mikopo yao, bali pia kuwalipa wafanyakazi pamoja na wasambazaji."

Ndadzungira alisema hadi sasa benki hiyo imeweza kutoa afueni kwa wateja zaidi ya 265, ikiwa ni kiasi zaidi ya shilingi bilioni 37 ya mikopo hiyo. Pia, alisema benki ya Stanbic imeendelea kutoa ushauri wa kifedha kwa wateja wake kuhakikisha wanakuwa na mkakati thabiti wa kuendeleza biashara.

"Tunawasisitiza wateja wetu wote ambao wanapitia changamoto za kifedha kutokana na uwepo wa Covid-19, kuwasiliana nasi haraka ili kwa pamoja tuweze kutafuta suluhisho madhubuti," aliongeza Ndadzungira.

"Kama benki tunaendelea kujizatiti katika kuleta matokeo chanya kwenye jamii tunayoihudumia na kuunga mkono serikali katika kudhibiti athari za kiuchumi zinazosababishwa na ugonjwa huu," aliongeza Ndadzungira.

# TIC yataka wawekezaji taarifa kila miezi sita

Na Romana Mallya

SERIKALI imewataka wawekezaji waliosajili miradi yao Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kuwasilisha taarifa za maendeleo na changamoto kila baada ya miezi sita ili ziweze kutatuliwa na kuboreshwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, aliyasema hayo jana baada ya kutembelea kiwanda cha OK Plast, kilichopo Vingunguti jijini Dar es Salaam.

Kiwanda hicho kimeajiri Watanzania 595 na wageni watano, kinachakata vyuma chakavu na kuzalisha rodi za shaba, nyaya za umeme, betri ingots na mikeka.

Waziri Kairuki alisema kanuni za usajili za TIC zinawataka wawekezaji kufanya hivyo ili kuweka ukaribu kati yao na kituo.

"Wawekezaji wote mliojisajili TIC pelekeni katika kituo hiki taarifa za maendeleo ya miradi yenu kila baada ya miezi sita ili tujue ni wapi kuna changamoto tuweze kuzitatua kwa wakati.

"Serikali ipo na ni sikivu na hii ni kwa nia njema. Nawapongeza kiwanda cha OK kwa ulipaji wa kodi na mmeajiri Watanzania wengi, niwaombe wamiliki wengine wa viwanda waige kutoka kwenu."

Meneja wa kiwanda hicho, Fadil Ghaddar, alisema uwekezaji wao kwa sasa umefikia Sh. bilioni 10 na tangu kuanzishwa kwake mwaka 2005 wamepata mafanikio ikiwa ni pamoja na kupata soko la ndani na baadhi ya nchi jirani ikiwapo Kenya.

Ghaddah changamoto yao kubwa ni upatikanaji wa malighafi za uzalishaji wa bidhaa na wameiomba serikali iweke mikakati ya kuhakikisha viwanda vya ndani vinazipata za kutosheleza.

"Serikali inaweza kuweka zuio kabla ya uuzwaji wa malighafi hizo nje ya nchi ili viwanda vya ndani viweze kujitosheleza na kuondokana na upungufu na kupunguza uzalishaji," alisema.

Alisema changamoto hiyo imewasababishia kupunguza uzalishaji kutoka tani 500 za shaba kwa mwezi hadi kufikia tani 150 pekee.

Alisema utafiti uliofanywa hivi karibuni na Taasisi ya BICO ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulionyesha kuna upatikanaji wa kutosha wa bidhaa chakavu za shaba Tanzania kiasi cha kutosheleza viwanda vya ndani.

"Tunakwama kupata malighafi hii kwa sababu inauzwa nje tunaomba serikali iliangalie suala hili," Ghaddar alimuomba Waziri Kairuki ambaye naye ameahidi kuliwasilisha mamlaka husika.

# Leseni za biashara kwa mtandao kuanza Mafinga

Na Joseph Mwendapole

HALMASHAURI ya Mji wa Mafinga Mkoa wa Iringa nayo inatarajia kuanza kutoa leseni za biashara kielektroniki baada ya kupokea vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Vifaa hivyo vilikabidhiwa jana kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Saada Mwaruka na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), Godfrey Nyaisa, katika makao makuu yake jijini Dar es Salaam.

Vifaa vilivyokabidhiwa ni kompyuta za mezani tatu, kompyuta mpakato moja, tambaza (scanner) moja, mashine ya kuchapishia (Printer) moja, modemu moja na simu za mkononi tatu.

Nyaisa alisema lengo kuu la kushirikisha halmashauri katika utoaji leseni kielektroniki ni kutengeneza mazingira rafiki kwa wafanyabiashara.

"Mfumo huu ni rahisi sana na unamwezesha mfanyabiashara kupata leseni akiwa popote pale. Mfumo huu utahitaji mfanyabiashara aweze kuweka viambatanisho vinavyotakiwa kisha ataweza kupata leseni yake," alisema.

Alisema katika hatua za awali mfumo huu unaweza kuwa na changamoto kadhaa kwa wafanyabiashara kutokana na matumizi ya mtandao, lakini anaamini wakipewa msaada wa karibu basi wataweza kuuzoea mfumo huu mapema.

Aliwataka pia kuusimamia vizuri mfumo wa utoaji wa leseni vizuri ili hata wakati utakapofika wa halmashauri zingine kuanza kutoa leseni kuwa mfumo huo basi ziweze kujifunza kutoka kwao.

Naye Kaimu Mkuu wa Idara ya Leseni Brela, Tawi Kilumile, alisema ili mfanyabiashara aweze kuomba na kupata leseni ya biashara kielektroniki inabidi atembelee tovuti ya www.Business.go.tz kisha kutengeneza akaunti na kuandaa ombi lake la leseni.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Saada aliishukuru Brela kwa kuwapatia vifaa hivyo na kuahidi kuvitumia kama ilivyo kusudiwa ili kuweza kutimiza lengo la serikali la kufikia uchumi wa kati.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Joketi Mwegelo (wa pili kulia), akikagua uzalishaji wa mavazi kinga (PPE), yanayotengenezwa hospitali ya wilaya hiyo, mkoani Pwani juzi, kwa ajili ya mapambano dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona ambapo sasa wana wagonjwa wawili. Kulia ni Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Stamford Mwakatage. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# DC Joketi aagiza watendaji usimamizi watoto kujisomea

Na Romana Mallya

MKUU wa Wilaya wa Kisarawe, Joketi Mwegelo, amewataka watendaji wa kata, kijiji, vitongoji na maofisa elimu wilayani humo kuhakikisha wanafunzi waliopo nyumbani kwa likizo ya corona wanajisomea badala ya kuzurura mtaani.

Mwegelo alitoa maagizo hayo juzi wakati wilaya yake ikipokea msaada wa vifaa vya kukabiliana na corona vilivyotolewa na Shirika la Plan International vyenye thamani ya Sh. milioni 76.8.

Alisema juzi (Jumatatu) aliyopita baadhi ya maeneo wilayani humo alishuhudia baadhi ya mitaa watoto wakiwa wanacheza kamari badala ya kuwa nyumbani wakijisomea.

"Tuendelee kuwahimiza watoto wetu wajisomee ili watakaporudi shule wasiachwe nyuma na wengine, nilifurahi baada ya kupita mtaa mmoja na kumkuta mtoto mmoja akiwa amekaa nje ya nyumba yao akijisomea," alisema.

Pia aliwataka viongozi katika wilaya hiyo kuhakikisha watoto wanalindwa hasa wa kike ili wajiepushe na mimba za utotoni.

Mwegelo aliitaka jamii kuhakikisha wazee wanalindwa ili wasipate maambukizo ya corona na kama ni huduma wahudumiwe wakiwa nyumbani.

Alisema katika wilaya yake tangu ugonjwa huo uanze hadi juzi ulikuwa na wagonjwa wawili pekee na kuitaka jamii pindi inapohitaji huduma za afya isiogope kufanya hivyo kwa sababu ya corona.

Naye, Meneja wa shirika hilo Kisarawe, Marcely Madubi, alisema wanafunzi kutoka kaya maskini wanaweza kukosa elimu ikilinganishwa na wale wanaotoka kwenye familia zenye kipato cha juu wanaosoma kupitia mitandao na runinga.

Pia alisema endapo wazazi watashindwa kubeba jukumu lao la malezi ya watoto, watoto wa kike wanaweza kuingia katika mimba za utotoni.

"Wazazi na walezi wahakikishe wanawaondoa watoto kwenye hali ngumu ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia na kuwabebesha majukumu mengine ya kifamilia wakati huu wakiwa majumbani badala ya kujisomea," alisema.

## SBL kushirikiana zaidi na serikali mapambano corona

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imeelezea utayari wake wa kuendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu maarufu kama Covid-19.

Hivi karibuni kampuni hiyo ilitoa jumla ya lita 1,250 za vitakasa mikono kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ukiwa ni mchango wake katika kupambana na ugonjwa huo hatari ambao mpaka kufikia sasa hauna chanjo wala tiba pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na wataalamu wa afya duniani.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma was SBL, John Wanyancha, alisema msaada huo ulikuwa ni mchango wa mara ya pili wa kampuni hiyo katika kupiga vita ugonjwa wa corona.

Wanyancha alisema SBL pia ilijitolea kusambaza vipeperushi vyenye ujumbe wa namna ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona sehemu mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu juu ya ugonjwa huo hatari.

"Kampuni ya SBL itaendea kushirikiana na serikali pamoja na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya ungonjwa wa corona. Tunawashauri umma na wateja wetu kuendelea kufuata taratibu za tahadhari zinazotolewa na Wizara ya Afya," alisema Wanyancha.

Ugonjwa huo wa homa kali ya mapafu uligundulika katika jimbo la Wuhan nchini China Decemba mwaka jana na umesambaa kwa kasi kubwa katika sehemu mbalimbali duniani, huku ukigharimu maisha na uchumi wa watu na mataifa mengi. Shirika la Afya Duniani (WHO) tayari limeshautangaza kama janga la kidunia.

# Tanzania, Kenya, Uganda zafundwa uzalishaji chakula

**Na Sabato Kasika**

KENYA, Tanzania na Uganda zimeshauriwa kuongeza uzalishaji wa chakula ili kutosheleza mahitaji ya raia wake ambao idadi yao inaendelea kuongezeka.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja Mradi wa Climate Resilient Agribusiness for Tomorrow (CRAFT), nchini Menno Keizer, kwamba kuna haja ya kujifunza kutumia uzalishaji unaoendana na mabadiliko ya hali ya hewa, kuvuna mazao kisasa na kuchakata mazao ni masuala ya uzalishaji wa chakula na mifumo ya kukisambaza.

Alifafanua kuwa ili kufanikisha ongezeko la uzalishaji wa chakula, kunahitajika ushirikiano wa wadau kufanya uwekezaji wa pamoja kuanzia wasambazaji, watoa huduma, wafanyabiashara kutoka sekta binafsi, na kuhakikisha kila mmoja katika nafasi yake anatekeleza wajibu wake ipasavyo.

"Kupitia mpango wa ubunifu kukabiliana na hali ya hewa na kusaidia kufanikisha uwekezaji, mpango huo utasaidia uwekezaji wa msingi wa utendaji ili kujenga nguvu ya kampuni za kilimo cha biashara kutoka sekta binafsi na watoa huduma ili kufanikisha kuongeza myororo wa thamani kwenye bidhaa zao," alisema Keizer.

Alisema kampuni nne za Tanzania (Nondo Investors Company Limited, Rogimwa Agro Company Limited, Jackma Enterprises Ltd na Mwenge Sunflower Oil Mills) zimesaini mkataba wa makubaliano wenye thamani ya Euro 567,135.

Keizer alisema Craft itapunguza hatari za kifedha za mipango mpya ya biashara ikiwa ni pamoja na zile za biashara za watu wa kati, wanawake na vijana, biashara za kilimo na za vyama vya ushirika, hivyo kuchangia kuongezeka kwa kiwango cha uwekezaji na ushiriki wa sekta binafsi katika mifumo ya chakula inayostahimili hali ya hewa katika Afrika Mashariki.

"Craft na washirika wake wawekeza zaidi ya Euro milioni mbili kuwezesha kuongeza uzalishaji wa chakula, kwani uwekezaji kupitia mradi huu umelenga kampuni na wakulima wanaojishughulisha na mazao ya alizeti, soya, ufuta, maharage, viazi na mtama na kuongeza myororo wake wa thamani wa mazao hayo katika nchi hizo," alisema.

Alisema, Craft nchini ni mradi unaoshirikisha sekta binafsi ukiwa na mikakati inayotambuliwa na mradi ili kufikia matokeo endelevu na kuongeza upatikanaji na uwapo wa chakula kuendana na hali ya hewa iliyopo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa (kulia), akikabidhi kompyuta mpakato kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Saada Mwaruka na vifaa ya Tehama kwa ajili ya utoaji wa leseni kimtandao katika halmashauri hiyo, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waandishi wasafiri Km. 70 kusaka 'nyungu'

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

WAANDISHI wa habari wa vyombo mbalimbali mkoani Morogoro, wameunga mkono kauli ya Rais Dk. John Magufuli ya kutumia mimea ya tiba mbadala kujifukiza ili kujikinga na ugonjwa unaosababishwa na maambukizo ya virusi vya corona nchini.

Waandishi hao wakiongozwa na Monica Lyampawe wa TBC, Idda Mushi (ITV) na Lilian Lucas (Mwananchi) walisafiri umbali wa kilometa 70 kutoka Morogoro Mjini hadi kijiji cha Kambala Mvomero kutafuata mimea hiyo.

Baada ya kukamilisha safari hiyo, Monica alisema kuwa wanakubaliana na kauli ya Rais ya kutumia mimea kujikinga na maradhi ya corona, hivyo wameamua kuitafuta mimea inayohusika nao waweze kujifukiza ili kupata kingamwili.

"Sisi wanahabari ni kioo kwa jamii kwa hiyo tumeamua kusafiri umbali mrefu hadi katika kijiji hiki cha Kambala kwa lengo la kutafuta mimea ambayo inatumia kujifukiza ili tuweze kujikinga na maambukizo ya corona," alisema Monica.

Alisema watatumia kalamu na fursa walizonazo katika jamii kuwaelimisha wananchi kutumia majani ya miti kujifukiza kwa kuwa ni njia sahihi ya kujiepusha na maradhi mbalimbali ikiwamo corona.

Kwa upande wake Idda, alisema anajisikia mwenye furaha baada ya kupata miti ambayo inatajwa kuwa ni ya kijifukiza ikiwa ni kitendo cha kuunga mkono kauli ya serikali ya kutaka watu kujikinga na corona.

"Nimeamua kuunga mkono kauli ya rais wangu ndiyo maana nimetembea umbali mrefu kwa lengo la kutafuta majani ya miti hii ili niweze kujifukiza, pia nitawashauri watu wengine kutumia njia hii kujikinga na corona," alisema Idda.

Lilian, alisema katika habari zake za kiuandishi ataendelea kuwahamasisha wananchi kutumia njia ya kujifukiza kwa kuwa ni njia sahihi ambayo ilitumiwa enzi za mababu na mabibi kujikinga na maradhi mbalimbali.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho, walieleza namna majani hayo wanavyo yatumia katika dawa na kwamba wao wamekuwa wakiyatumia kila wanapoona kuwa miili yao inasumbuliwa na maradhi.

Kashunga Mora, miongoni mwa wakazi wa kijiji hicho, alisema wananchi wengi wa hapo ambao ni wafugaji wanatumia majani ya mimea kijifukiza kama dawa kitendo ambacho kimekuwa kikiimarisha afya zao.

## Wenye ulemavu kuimarishiwa huduma

OFISI ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi na umma, inaandaa Mpango wa Taifa wa kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu wa mwaka 2020/21 - 2023/24.

Ofisi hiyo ilitoa kauli hiyo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau, ambaye alisema kumekuwa na utekelezaji mdogo wa huduma za watu wenye ulemavu kwenye huduma za majengo, vyombo vya usafiri pamoja na vyombo vya habari.

"Je, serikali inasema nini katika kuhakikisha huduma za watu wenye ulemavu zinazingatiwa," alihoji.

Ikijibu, ilisema moja ya lengo mahsusi la kuanzishwa kwa mpango huo ni kuimarisha mazingira ya upatikanaji na ufikiwaji wa huduma mbalimbali za jamii yenye kuzingatia mahitaji yao ikiwamo elimu, afya, hifadhi ya jamii, usafiri, barabara, michezo, burudani, vifaa saidizi, marekebisho, taarifa na mawasiliano.

Ilisema serikali ilipitisha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namba 9 ya Mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2012.

"Kifungu cha 35 – 50 cha sheria hiyo kinaelekeza kufikika kwa majengo, mazingira yanayotuzunguka na upatikanaji wa huduma na habari kwa watu wenye ulemavu," ilisema.

Ilifafanua kuwa serikali ilifanya mapitio ya kanuni za maudhui ya vyombo vya habari za mwaka 2011 kinachovitaka vyombo vyote vya habari kuwa na wakalimani wa lugha ya alama.

"Baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa vikitekeleza agizo hili mfano, Televisheni ya Taifa (TBC) na Uhai Tv (UTV)," ilisema.

Vile vile, ilisema serikali inaendelea kufuatilia suala hilo ili kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya habari vinatekeleza agizo hilo.

"Kwa upande wa majengo, serikali imeweka mwongozo wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ukaguzi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2017 ambao umezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu," ilisema.

Ilisema serikali inaendelea kusimamia kuhakikisha sekta zote zinazingatia uwapo wa huduma bora za wenye ulemavu.



# Kinamama wanaojifungulia vituoni waongezeka

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa idadi ya kinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma imeongezeka hadi kufikia asilimia 83 mwezi Machi 2020.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Josephine Genzabuke.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema asilimia 75 ya vifo vya kinamama vinavyotokea wakati wa ujauzito na kujifungua vinaweza kuepukika.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kinamama hasa waishio vijijini wanajifungua salama?" Alihoji.

Ikijibu, ilisema katika mwaka 2015/16 kulikuwa na kinamama asilimia 64 waliokuwa wanajifungulia kwenye vituo hivyo, lakini hivi sasa idadi imeongezeka na kufikia 83.

Pia, ilisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi imeboresha vituo vya afya zaidi ya 352, na vingine kujengwa upya.

"Lengo ni vitoe huduma zote za afya ya uzazi kabla na wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua ikiwamo kumtoa mtoto tumboni kwa njia ya operesheni, na kuzijengea uwezo wa kutoa huduma ya damu salama kwa watakaohitaji," ilisema.

Ilisema hospitali mpya 67 za halmashauri zinajengwa ili huduma ziwafikie wananchi wote wa vijijini na mijini kwa usawa na urahisi zaidi.

"Katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa na vifaa tiba vinakuwapo muda wote, serikali imeongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba, kutoka Sh. bilioni 31, mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 200 mwaka 2019/20," ilisema.

Ilieleza kuwa ongezeko hilo la bajeti na usimamizi imara wa rasilimali limeongeza upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 53 kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 94 kwa 2019/2020.



Juhudi hizo zimewezesha wajawazito kuendelea kupata huduma za afya ya uzazi na mtoto ikiwamo kinga tiba dhidi ya malaria (SP), Fefol ambayo ni kinga tiba dhidi ya upungufu wa damu, vipimo vya shinikizo la damu, kaswende, wingi wa damu na sukari.

Kadhalika, ilisema Novemba 6, mwaka 2018, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alizindua kampeni ya "Jiongeze tuwavushe salama" ambayo ni ya kitaifa inayolenga kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini Tanzania.

"Madhumuni ya kampeni ni kuhamasisha viongozi wa serikali, wa dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, wadau wa maendeleo, watoa huduma za afya, familia na jamii kwa ujumla ili kuchangia juhudi za taifa za kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga," ilisema.

Ilibainisha kuwa wakuu wa mikoa walisainishwa mikataba ya utekelezaji na ufuatiliaji katika mikoa yao.

# Ajali barabarani zasababisha vifo 1,772

SERIKALI imesema katika kipindi cha Juni 2018 hadi Aprili, 2020, jumla ya ajali za barabarani 3,500 zimetokea na kusababisha vifo vya watu 1,772.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mtambile (CUF), Masoud Abdallah Salim.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema ajali za barabarani na majini zimekuwa zikisababisha vifo na majeruhi.

"Je, ni watu wangapi wamepoteza maisha kwa ajali za barabarani na majini kuanzia kutoka Juni, 2018 hadi sasa," alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema kati ya ajali hizo vifo ni 1,772 na majeruhi 4,906.

Kwa upande wa ajali za majini kwa kipindi kama hiki kuanzia mwezi Juni, 2018 hadi Aprili, 2020 zimetokea ajali 17 zilizosababisha vifo vya watu 244 na majeruhi 41.



ALHAMISI MEI 21, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Dawasa na jumuiya za maji katika ubia kukabili corona**




Ukurasa 13

Hofu ongezeko mimba kwa wanafunzi likizo ya corona



Ukurasa 14

**Ijue shida ya utapiamlo na undani wake**

AFYA

# DC: Tutawapima wanafunzi wote baada likizo ya corona

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

NI takriban miezi mitatu, tangu ugonjwa wa corona kuingia nchini. Serikali baada ya kuona mambo sivyo, iliagiza kufungwa kwa shule na vyuo, ni kuwabakisha majumbani wanafunzi, kuwaepusha wasipate maambukizo ya ugonjwa huo.

Kukaa nyumbani ni moja ya jitihada za kuwapunguzia wanafunzi wasirundikane katika madarasa, hosteli au bwenini, iwe vyuoni au shuleni.

Katika kuepuka ugonjwa huo, kikubwa kinaelezwa ni kukwepa mikusanyiko, hivyo wanafunzi wakatakiwa kutoendelea na masomo kutokana na mikusanyiko.

Pamoja na katazo hilo, bado kuna baadhi ya maeneo watoto wadogo ambao ni wanafunzi, bado wanazurura ikiwamo katika baadhi ya masoko na vituo vya daladala, wakiendelea na biashara ndogo.

Siku chache zilizopita, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mkuranga, alieleza kusikitishwa na baadhi ya wazazi wanaowaruhusu watoto wao kufanya biashara ndogo katika maeneo mbalimbali ya wilaya, badala ya kutulia nyumbani.

"Kupitia viongozi wetu, tunatakiwa maagizo tuyatii. Watoto wakae nyumbani, wasijiingize katika makundi, pia hata biashara wanazofanya sio sahihi," anasema.

Anaongeza kutokana na ukweli kwamba baadhi yao wanaishia kuzurura mitaani, wanatarajia shule zitakapofunguliwa; msingi na sekondari, watawapima ujauzito.

Pia, Sanga anatoa agizo kwa watendaji wa kata zote wilaya kwake, kwamba waendelee kutoa elimu ya afya na uzazi kwa wazazi na walezi wa wanafunzi hao wa shule, ikilenga mahsusi kuwaepusha na mimba zisizotarajiwa hasa kipindi hiki cha mapumziko ya kupisha janga la corona.

Anaeleza kusikitishwa na baadhi ya wazazi wanaokaidi agizo la kiserikali, ambalo linawasaidia watoto kubaki nyumbani na wakati huohuo, wakijiepusha na vitendo vitakavyoathiri elimu yao, shule zitakapofuguliwa.

Sanga anaitaka jamii iendelee kuchukua hatua kuhusu kujikinga na ugonjwa huo, serikali ikiendelea kuwaunga mkono kwa kuielimisha jamii namna ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Anataja msaada mwingine ni vitakasa mikono vilivyopo katika maeneo mbalimbali yenye mwingiliano wa watu wanakofika kupata mahitaji hasa ya lazima, kama vile hospitali na sokoni.

Pia, ana rai anayowaendelezea wananchi kuendelea kuvaa barakoa, huku madiwani waendelee kuwahamasisha kuchukua tahadhari zinazohusu ugonjwa huo.

Sanga anasema, kuibuka corona isiwe kigezo cha watu kushindwa kuwahudumia wananchi kwa kukaa majumbani, bali kinachotakiwa ni kutoogopa ugonjwa, huduma ziendelee zinavyokusudiwa.



Wanafunzi wa eneo la Vikindu, Mkuranga katika moja ya matukio ya ugeni uliowahusu. **PICHA: MTANDAO.**

> **Watoto wakae nyumbani, wasijiingize katika makundi, pia hata biashara wanazofanya sio sahihi.**

**X- RAY YATUA**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Juma Abeid, anazungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani, kwamba kuna hatua waliopiga kwa serikali kuu kuwapatia huduma za X-ray katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga.

Mwenyekiti Abeid, anasema kabla ya msaada huo uliotolewa na Rais Dk. John Magufuli, na wagonjwa waliendа kupata huduma hiyo nje ya wilaya na hasa mkoa jirani, kwenye Jiji la Dar es Salaam.

Mwenyekiti huyo kupitia nafasi yake, ni miongoni mwa waliofanikisha zahanati na vituo vya afya kujengwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Wilaya ya Mkuranga.



Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga. **PICHA: YASMINE PROTACE**

MAZINGIRA

# Dawasa na jumuiya za maji katika ubia kukabili corona

• Maji tiririka kwa wingi, ndoo, sabuni...

**Na Mwandishi Wetu**

MBINU mojawapo katika kukabiliana na na maambukizo ya virusi vya corona, watu kujikinga kwa kunawa mikono wakitumia majisafi yanayotiririka na sabuni, kwa sekunde zisizopungua 20.

Hiyo ni kati ya njia muhimu zinazosisitizwa na wataalamu wa afya, pamoja na serikali katika kukabiliana na maambukizi hayo ya homa inayoshambulia mapafu, maarufu corona.

Katika mustakabali huo, ni wazi mahitaji ya maji na umuhimu wake katika mapambano yameongezeka, hivyo watoa huduma za maji wote jijini Dar es Salaam, ni wahusika wakuu katika vita hivyo.

Mamlaka ya Majisafi na Mazingira, jijini Dar es salaam (Dawasa), waliwaita katika ofisi zake kuwapa elimu inayohamasisha kuunga mkono jitihada za serikali kupambana dhidi ya maradhi hayo, kwa wanaotoa huduma.

Dawasa kwa sasa inahudumia mkoa wa Dar es Salaam na miji jirani ya Bagamoyo, Kibaha, Mkuranga, Kisarawe na Chalinze, ikibeba jukumu la msimamizi wa miradi ya umma inayoendeshwa na jamii kupitia ama jumuiya za watumia maji au kamati za maji.

Jijini Dar es Salaam, kwenye wakazi wanaokadiriwa milioni tano, kuna jumla ya watoa huduma za maji zaidi ya 75, chini ya usimamizi wa Dawasa.

Katika hatua yao wameweka vifaa kinga kwenye maeneo yenye mikusanyiko. Hiyo ni pamoja na ndoo za maji kwa ajili ya kunawa mikono na sabuni kwenye maeneo zaidi ya 241.

Hadi sasa, maeneo yaliyofikwa na mpango huo ni katika ofisi za umma za kihuduma, vituo vya mabasi, vituo vya waendesha bodaboda, teksi, masoko, hospitali, magenge, vituo vya afya, kwa waendesha bajaji na kwa wanaochota maji.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mawasiliano na Jamii, Neli Msuya, Dawasa inasimamia miradi ya kijamii iliyokuwa inaendeshwa na manispaa za Jiji la Dar es Salaam, chini ya kamati za maji za wananchi katika maeneo mbalimbali, takribani jumuiya 321.

### WENYEVITI WA JUMUIYA

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maji ya Mamboleo A, wilayani Temeke, Ally Saidi, anakubali kuwapo mwitikio mkubwa wa jamii, katika suala zima la kunawa mikono kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya corona.

"Kwa kweli, baada ya maelekezo ya serikali kuhusu kuweka vifaa kinga kwenye maeneo muhimu ya kihuduma wananchi wengi wamepokea hili jambo kwa haraka zaidi na kwa mwamko mkubwa sana.

"Dawasa, pia walituelimisha namna bora ya kujikinga kwa kupitia huduma ya majisafi ambayo sisi tunaisimamia chini ya mamlaka hiyo katika maeneo yetu," anasema.

Hali iliyoko sasa, Said anafafanua kwamba kila kituo kilichopo chini ya mradi wa maji kimeweka ndoo na sabuni kwa ajili ya kuwawezesha wahitaji wa huduma ya maji ya kunawa mikono, kabla ya kushika bomba. Kiongozi huyo wa mradi wa kijamii wa maji, anafafanua kuwa hatua ya uwekaji ndoo na sabuni haikuishia katika huduma za maji, bali wamezisambaza katika maeneo mbalimbali yenye mkusanyiko wa watu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumia Maji Moringe, Mbagala Kizuiani wilayani Temeke, Yusufu Chilala, anasema wameweka utaratibu kuhakikisha kila anayefika kwa ajili ya kupatiwa huduma ya maji katika vizimba husika, ni sharti anawe mikono kwa sabuni katika ndoo iliyowekwa pembeni, vinginevyo hatopata huduma.

"Hivi sasa ujanja ni kunawa mikono na sabuni ndipo upate huduma. Huwezi kushika koki ya kwenye vizimba bila ya kunawa mikono yako na sabuni, usipofanya hivyo huwezi kupata maji.

"Tunaishukuru Dawasa, wametukabidhi vitendea kazi vya namna ya kujikinga na corona, ikiwamo ndoo na sabuni na elimu sahihi ya kutumia," anasema Chilala.

Anafafanua kuwa Dawasa imewaruhusu kuunganisha maji kwa wananchi, mtazamo ni kuwahakikishia wanapata huduma ya kunawa mikono kwa maji safi yanayotiririka.

Kwa mujibu wa Chilala, hatua ya Dawasa kuwapa vifaa imewaongezea nguvu katika utekelezaji majukumu yao kwa ufanisi katika utoaji huduma, wakizingatia tahadhari zote dhidi ya maambukizo ya corona.

### WAKAZI

Rukia Simba, mkazi anayepata huduma ya maji kupitia jumuiya hiyo, anasifu upatikanaji maji uliopo, kwani unpatokana kiasi kikubwa katika kilichopo cha mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Hatua hii ni nzuri sana kwetu ambao hatuna maji ya mtandao wa Dawasa na ambao tunahudumiwa na jumuiya hizi za maji. Ugonjwa huu ni hatari sana na bila uhakika wa upatikanaji wa maji, basi hali ingekuwa mbaya zaidi.

"Wataalamu wa afya wanatuambia tunawe kwa maji ambayo yanatiririka kwa sekunde zisizopungua 20, sasa kama maji ni ya shida tungewezaje sasa unafikiri?" Anahoji.

"Kwa sasa mambo ni mazuri na huwezi kupata huduma ya maji kama hujanawa mikono yako na sabuni kwenye ndoo iliyotengwa kwenye vizimba vya kuchotea maji.

"Kwa kweli ni utaratibu mzuri kwa sababu unawakinga wananchi dhidi ya corona kama serikali ilivyoagiza. Kama unataka kuteka maji, lazima unawe mikono yako na sabuni kisha upate huduma.

"Tunaishukuru Dawasa imerahisisha mchakato huu kwa kutoa sabuni na ndoo zaidi ya 40 katika eneo letu," anasema Rukia, katika ufafanuzi wake wa ziada.

### SAUTI DAWASA

Neli anasema, jumuiya za maji zimekuwa msaada mkubwa kwao katika utoaji huduma za maji kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa Dawasa, huku zikisimamiwa kwa karibu na mamlaka hiyo.

"Kwa kipindi hiki cha mapambano dhidi ya virusi vya Covid-19, tumejizatiti kuhakikisha jumuiya hizi za maji zinakuwa mstari wa mbele katika kujikinga dhidi ya maambukizo na vilevile kuwakinga watumiaji huduma zao wanaopata maji kupitia vizimba vilivyowekwa.

"Tumewapa vifaa kinga ambavyo ni ndoo za kunawa, sabuni pamoja na elimu juu ya usahihi wa kunawa mikono na tahadhari nyingine kwa kipindi hiki," anasema Neli.

Anasema, hadi sasa Dawasa inaendelea na mpango wa kusajili watoa huduma za majisafi binafsi, waliokidhi vigezo, ikiwamo kibali cha matumizi ya maji ardhini kutoka Mamlaka ya Bonde la Wami Ruvu na ubora wa maji yenyewe.

Kwa mujibu wa Neli, Dawasa inawezeshwa na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019, ikiwa na upekee wa jukumu la kusimamia huduma ya maji na usafi wa mazingira jijini Dar es Salaam.



Mkazi wa Mamboleo A, akisafisha mikono yake kwa kutumia maji na kitakasa mikono kabla ya kuyachota katika bomba la jumuiya hiyo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> **Wataalamu wa afya wanatuambia tunawe kwa maji ambayo yanatiririka kwa sekunde zisizopungua 20, sasa kama maji ni ya shida tungewezaje sasa unafikiri?**



Ndoo ya kunawa maji na kitakasa mikono, zikiwa katika bomba la Jumuiya ya Maji ya Mamboleo A, iliyopo wilayani Temeke.

AFYA

# Hofu ongezeko mimba kwa wanafunzi likizo ya corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

• Mkoa wajipanga kila kona, kwa ishara ya janga




Wasichana wa Shinyanga wakiwa katika tamasha maalum linalowahusu. **PICHA: MTANDAO**

UNAPOTAMKA kilio cha mimba za utotoni, hapana shaka jicho na kidole kikuu cha lawama 'namna moja' kiko kwa mkoa wa Shinyanga.

Hapo kuna mimba lukuki za watoto, vivyo hivyo kwa ndoa zao. Moja ya sababu kuu inatajwa kuwa wazazi na walezi wanatekwa na tamaa ya mbadala wa mifugo.

### ALIVYOJIPANGA DC

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, hakubaliani nalo hata kidogo, nakuja na uamuzi mgumu katika eneo lake la utendaji, akiongozwa na mtazamo 'bora lawama kuliko fedheha.'

Anatekeleza hilo kwa mtindo wa kuhamasisha mashirika na watendaji wa serikali, kuanzia kwenye kitongoji, kijiji na kata kueneza darasa wazazi na walezi waachane na ndoa za utotoni, hasa katika kipindi kilichopo 'likizo ya corona' walio nayo wanafunzi hivi sasa.

Tahadhari ya Mkuu wa Wilaya huyo ni kwamba, kuna uwezekano baadhi ya wazazi kutumia mwanya huo kuozesha watoto wao ndoa za utotoni, ili wapate mifugo, kwa sababu ya likizo kuwa ndefu, jambo litakalozima ndoto za wanafunzi.

"Natoa onyo kwa wazazi na walezi wasiozeshe watoto wao ndoa za utotoni katika kipindi hiki cha likizo ya corona na yule ambaye atabainika kufanya hivyo, serikali itamchukulia hatua kali za kisheria," anaonya Mkuu wa Wilaya kwa ukali.

Anageuza uso kwa wadau akiendelea: "Mashirika ambayo mnatoa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona katika maeneo ya vijijini, toeni pia na elimu ya ukatili kwa wananchi, ikiwamo wazazi wasiozeshe watoto wao ndoa za utotoni, ili shule zitakapofunguliwa wote warudi shule na kutimiza ndoto zao."

### POLISI NAO?

Mtekelezaji wa maagizo hayo ya Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama Wilaya, Kamanda wa Polisi Mkoa (RPC) wa Shinyanga, Debora Magiligimba, anavalia njuga mimba na ndoa za utotoni, akiwa mahsusi na kitendo cha wazazi kuogesha watoto wao dawa za mvuto wa kimapenzi.

Anaeleza, mtazamo wa wana Shinyanga unazama mbali katika kupata wachumba, ili waozeshwe kwa mbadala wa mifugo kwa wazazi na walezi.

"Nilipokuja hapa mkoani Shinyanga mwishoni mwa mwaka jana (2019), kulikuwa na tatizo la mauaji yatokanayo na imani za kishirikina, ambalo nimelipunguza na kubakia tatizo la mimba na ndoa za utotoni, hasa katika Wilaya ya Kishapu.

"Ikabidi nikae na viongozi wa dini, watendaji wa vijiji na kata kuzungumzia tatizo hili, nikaambiwa tatizo kubwa ni mila na desturi za uogeshaji watoto wa kike dawa za mvuto wa kimapenzi, pamoja na mnada kuwa kichocheo cha ngono zembe," anafafanua Kamanda.

Pia, anawaonya wote ambao ama watawapatia ujauzito wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni, jeshi hilo halitakuwa na huruma nao, wataangukia mikono ya sheria.

Davis Msangi ni Mkuu wa Upelelezi (RCO) mkoani Shinyanga, anajazia hoja hiyo kwa tahadhari kwa wazazi, akiwataka wasiwaozeshe watoto wao katika umri mdogo, ili waweze kutimiza ndoto zao, pia tahadhari zao kiafya.

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya Mwaka 2002, pia Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka, inamwingiza kwenye kifungo cha muda mrefu, mtu anayethibtika kushiriki ngono na ama binti mwanafunzi au anayeangukia umri chini ya miaka 18.

> "Pia, tutakuwa tukitoa elimu kwa wazazi ya kuacha kuozesha watoto wao ndoa za utotoni, bali wawaache wasome ili watimize ndoto zao na kuja kuwasaidia hapo baadaye.

### MTEKELEZAJI KAMPENI

John Myola, Mkurugenzi wa Shirika la Agape, mtekelezaji wa mradi wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni katika Halmashauri ya Wilaya za Shinyanga na Kishapu, anasema katika kipindi kilichopo wanafunzi wakiwa likizo.

Kwa mujibu wa mkuugenzi huyo, hivi sasa wanalenga kujikinga na maambukizo ya virusi, wakipitia elimu ya kuzuia mimba kwa wanafunzi.

Anasema, wataanza kutoa elimu hiyo katika Kata ya Mwamala, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, eneo wanakotekeleza mradi wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, kuwalinda wanafunzi ama wasipate au kuozeshwa.

"Shirika letu la Agape, mbali na kuanza kutoa elimu kwa wananchi ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona na kugawa vifaa vya kujikinga.

"Pia, tutakuwa tukitoa elimu kwa wazazi ya kuacha kuozesha watoto wao ndoa za utotoni, bali wawaache wasome ili watimize ndoto zao na kuja kuwasaidia hapo baadaye," anaeleza Myola.

"Katika kipindi hiki cha janga la maambukizo ya virusi vya corona tukiendelea kukaa kimya na kutopiga kelele, tutajikuta shule zikifunguliwa watoto wengi wasiende shule sababu ya kupewa ujauzito au wengine wameshaozeshwa na wazazi wao ndoa za utotoni," anaongeza.

### OFISA USTAWI

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, anaonyesha shaka kwamba katika 'likizo ya corona' huenda kukatokea ongezeko la ujauzito na ndoa za wanafunzi, sababu ni usimamizi duni, akidai mabinti kuzurura ovyo mitaani.

Anasema uzururaji ovyo wa watoto mitaani hasa kwa watoto wa kike wanakuwa katika hatari kubwa ya kupewa mimba, sababu kuu ni kukosa uangalizi, huku wazazi wanajawa na tamaa ya mifugo, kwa kuwanadi mabinti kwa wanaume, hawapo tayari kuwaona nyumbani muda wote.

"Nimeagiza maofisa ustawi wa jamii kila wilaya mkoani hapa, kutoa elimu kwa wananchi hasa katika kipindi hiki cha wanafunzi, ambao wapo katika 'likizo ya corona' watoe elimu ya wazazi, wasiozeshe watoto ndoa za utotoni, pamoja na kuondoa watoto wote wanaozurura ovyo mitaani," anasema Lydia.

### WADAU

Katibu Mpango Mkakati Kitaifa wa Serikali wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto Mkoa wa Shinyanga (Mtakuwwa), Tedson Ngwale, anasema mkakati uliopo serikalini ni kuendelea kupunguza mimba na ndoa za utotoni na elimu kwa jamii, kuhusu madhara yaliyopo.

Ngwale anataja takwimu za mimba za utotoni Shinyanga kuanzia mwaka wa fedha uliopita (Julai 2018 hadi Juni 2019), kuna watoto 168 waliopewa mimba na kuacha masomo.

Anataja mgawanyiko wake, kuna jumla ya shule za sekondari 161 na msingi saba na katika mwaka huo wa fedha, jumla ya wanafunzi 32 wameolewa ndoa za utotoni na kubainisha kuwa hofu yake kwa mwaka huu (2020) huenda takwimu zikaongezeka.

Katibu Mipango huyo, anaelekeza hofu ya watoto watakaa nyumbani kwa muda mrefu nyumbani, inaweza kuwaacha pabaya.

AFYA

# Shida ya ugonjwa utapiamlo na undani wake unavyotesa

**Na Mwandishi Wetu**

UTAPIAMLO si msamiati mgeni kwa jamii. Asasi ya Reichet Fundation ya nchini katika tovuti yake inatafsiri: "Ni ugonjwa unaoathiri kukua kwa mwili na akili ya mtoto (na mtu mzima)."

Ni namna ya mwendelezo wa kinachosemwa kimataifa, ikiwamo kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) na Shirika la Chakula la Kilimo Duniani (WHO).

Kimsingi, ni maradhi yenye tabia ya kumjengea mtoto wasifu kadri anavyozidi kukonda, macho na utosi wa kichwa hubonyea, ngozi na mishipa ya mwili inakauka na uwezo wa kudhibiti joto mwili hupungua.

Chanzo chake kikuu ni ukosefu wa vitamini na madini ya kutosha mwili, ikiangukia zaidi kwa namna mbili: Mosi ni, ukosefu wa protini, nishati, vitamini na madini mwilini, pili kuwapo maambukizo ya kila mara ya maradhi kwa mtu.

"Magonjwa kama vile kuharisha, surua, malaria, na magonjwa ya kupumua hudhoofisha mwili sana na kupunguza vitamini na madini. Magonjwa hayo humfanya mgonjwa apoteze hamu ya kula naye hula chakula kidogo sana na hivyo anapata utapiamlo.

"Kwa upande mwingine, mtoto asiyepata chakula cha kutosha anaweza kuambukizwa magonjwa kwa urahisi. Jambo hilo huongeza idadi ya watoto wanaokufa kwa sababu ya kukosa vyakula vinavyojenga mwili," zinafafanua taarifa za wadau wa afya kimataifa.



Mtoto mwenye utapiamlo, katika moja ya maeneo yaliyokumbwa na vita barani Afrika. **PICHA: UMOJA WA MATAIFA**

**VIPI MTOTO?**

Watoto wanakua haraka na hivyo wanahitaji nishati na protini nyingi zaidi. Vivyo hivyo, wajawazito na wanaonyonyesha wanaweza kuupata utapiamlo.

Mtoto mchanga huanza kuathiriwa akiwa tumboni, sababu kuu ni mama anapokosa chakula cha kutosha au kilicho bora kabla na wakati wa mimba, hata akijifungua mtoto mwenye uzito mdogo.

'Kichanga' anapoachishwa kunyonya mapema na akakosa lishe stahiki na kichafu, mama huyo naye anaweza kuangukia katika utapiamlo.

Utapiamlo unamwathiri mtoto kwa njia nyingi, ikiwamo ukuaji, mathalani anapokosa madini ya kutosha hasa chuma, aiodini, zinki na vitamini hasa vitamini A, kunamuweka pabaya mtoto kiafya.

Kwa nini sasa inawashambulia watoto? Ni kwa sababu wanakua haraka, hivyo wanahitaji nishati na protini nyingi zaidi. Vivyo hivyo kwa wajawazito na wanaonyonyesha.

Mtoto mchanga anaathirika kuanzia tumboni, iwapo mama hatopata chakula cha kutosha, kabla au na wakati wa ujauzito.

> **Pia, mlo wa vyakula vilivyoimarishwa na kampeni mbalimbali za lishe kimataifa na mamlaka za kiafya, zinatajwa kuwa na maana kubwa kwa uhai wa binadamu.**



Mtoto mwenye afya njema, akipatiwa mlo kwa utaratibu. **PICHA: MTANDAO**

Pia, hutokea mtoto anapoachishwa kunyonya mapema, asipolishwa vizuri, au usafi usipozingatiwa, anaweza kuugua utapiamlo.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), linasema ukosefu wa vitamini A kumewaathirti watoto wachanga milioni 100 duniani, wakapata upofu na kudhoofisha mfumo wao wa kinga, hivyo kuwapunguzia uwezo wa kujikinga na maambukizo.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa, inarejea madhara ya utapiamlo mwilini, kama vile moyoni, figo, tumbo, mapafu na ubongo na uchunguzi unaonyesha, makuzi duni ya mtoto yana athari za kudumu akilini.

Hata hivyo, Unicef inakiri jitihada zinazofanyika kwa kauli: "Zaidi ya robo tatu ya watu wanaokufa kutokana na magonjwa yanayohusiana na ukosefu wa chakula, hufa kwa sababu ya utapiamlo mdogo au wa wastani."

**VYANZO KIJAMII**

Kuna mambo mengine ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kimazingira yanayochangia kuwa visababishi vya utapiamlo.

Vilevile kunatajwa mgawo duni wa chakula kwa kuwabagua kinamama na kuwanyima fursa za elimu rasmi na zisizo rasmi na athari za mazingira kusababisha uhaba wa chakula.

Ripoti ya Hali ya Uhaba wa Chakula Duniani ya mwaka 2001, ilionyesha kati ya Oktoba mwaka 1999 na Juni, 2001, nchi 22 duniani ziliathiriwa na ukame; vimbunga au mafuriko nchi 17; nchi 14 vita vya wenyewe; huku migogoro nchi 3 na mbili, matetemeko ya ardhi.

**MZIZI MKUU**

Asasi za kimataifa zikiwamo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia wa Watoto (Unicef) na Shirika la Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (WHO), zinaorodhesha vyanzo vyake katika maeneo makuu matatu.

Kunatajwa kuwapo vyanzo vya karibu: Hapo ni kama ukosefu wa pesa; uzalishaji mdogo wa chakula; matunzo na uhifadhi duni wa vyakula; uchaguzi usio sahihi wa vyakula, mpango, usimamizi na matumizi yasiyo sahihi ya mapato na ulishaji duni. Hiyo inahusu zaidi watu wazima.

Aidha, kuna mtazamo kwa wanaonyonyesha, wagonjwa na wazee; Inabeba mitazamo kama maandalizi duni na usafi, kinga na tiba ya magonjwa na matumizi ya huduma za afya.

Kurejea, andiko la kimataifa la mwaka 2004 la Unicef na WHO, liitwalo 'Unicef Framework in FAO (2004) Family Nutrition Guide' pia, lina ufafanuzi kuhusu mchango wa umaskini na maisha duni, kuukaribisha utapiamlo.

Ni ripoti inayotoa viashiria vya uhalisia wa maisha duni kama vile kutumia maji kidogo kuliko mahitaji, mazingira ya dhiki, msongamano wa makazi na huduma duni za afya, vyote vina nafasi yake.

Mengine yanaangukia katika umaskini uliokithiri kwa jumla na ukosefu wa fursa za ajira; usawa katika mgawanyo na udhibiti wa rasilimali katika jamii, wilaya, nchi na ngazi za kimataifa.

Sambamba na hiyo, mashirika hayo ya Umoja wa Taifa yanataja ukosefu wa elimu kwa kinamama, msongamano, uharibifu wa mazingira; machafuko na migogoro ya kisiasa; ukosefu wa huduma za afya, elimu; na ubaguzi katika jamii.

**LISHE BORA**

Lishe bora inaangukia pia katika vyakula vilivyoimarishwa. Hapo inatajwa ni vyenye nyongeza ya virutubisho ambavyo, kupitia lishe za kawaida kama vile vya kila siku, ikiwamo unga, nafaka na mafuta yatokanayo na mimea, sukari na chumvi, huku viazi vitamu vyenye rangi ya chungwa na manjano, wataalamu wanavitaja kuwa na utajiri wa Vitamini A.

Pia, mlo wa vyakula vilivyoimarishwa na kampeni mbalimbali za lishe kimataifa na mamlaka za kiafya, zinatajwa kuwa na maana kubwa kwa uhai wa binadamu.

**WALAKINI**

Hata hivyo, ripoti za uchambuzi huo, unataja walakini kwamba, vyakula vilivyoboreshwa mara zote haviwafikii walengwa kutokana na aina ya mahitaji ya kila mlaji kuwa tofauti.

Wadau hao wa afya wa kimataifa, wanafafanua kwamba vyakula vingi kwa sasa vimeimarishwa kulingana na mahitaji ya mtu mzima.

Kwa vile mahitaji ya virutubisho hutofautiana kulingana na umri na afya ya mtumiaji, vyakula vilivyoimarishwa havitoshelezi mahitaji ya kila mtu na havitoi kiwango kinachohitajika kwa ajili ya watoto au wajawazito, kusaidia ukuaji na uzazi.

Pia, kupatikana vyakula hivyo bado ni tatizo kwa sababu vyakula hivyo hupatikana kwa wale wanaoweza kununua vyakula vilivyohifadhiwa.

***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa taarifa za kimataifa.***



## HABARI DODOMA

## Walengwa Tasaf kulipwa ruzuku kwa mtandao

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) Ladislaus Mwamanga, amesema kuwa katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya Tasaf, ruzuku kwa walengwa wa kaya maskini, zitafanyika kwa njia ya mtandao nchi nzima.

Aidha, katika kipindi hiki cha pili kitatumia jumla ya Sh. trilioni 2.032 ambazo zitatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha miundombinu ya afya, elimu, maji, na sehemu nyingi itatumika kutoa ruzuku.

Pia katika kipindi hiki cha pili kaya zote zitafikiwa ikiwa ni pamoja na walengwa ambao hawakufikiwa katika kipindi cha kwanza.

Mwamanga aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malipo ya walengwa wa kaya maskini kwa mfumo wa mtandao nchi nzima.

Alisema kuwa baada ya kukamilika kwa kipindi cha majaribio na kuona faida za mfumo huo uongozi wa Tasaf, umeamua kwamba katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ruzuku kwa walengwa itafanyika kwa njia ya mtandao.

"Hivyo walengwa wote wanatakiwa kujiandikisha na kupata kitambulisho cha Taifa kilichotolewa na Nida, ili kuweza kufungua akaunti ya simu au benki yenye jina halisi la mlengwa," alisema Mwamanga.

Aidha, alisema wakati wa kuchagua mtandao wa simu mlengwa ahakikishe mtandao wa simu anaochagua uwe unapatikana kwa ufanisi kwenye eneo analoishi na pia awepo wakala wa mitandao ya simu mwenye uwezo wa kutoa huduma kwa watu wengi bila usumbufu.

"Kuwa na kitambulisho cha Nida na namba ya simu iliyosajiliwa au akaunti ya benki ndiyo vitu pekee vitakavyowezesha mlengwa kulipwa ruzuku," alifafanua Mwamanga.

Pia, alisema walengwa wanasisitizwa kuwa ni muhimu kuwa na simu zao binafsi ili kuepusha kufungiwa laini zao kama hawatazitumia kwa muda mrefu.

Mwamanaga, alisema walengwa wote wanakumbushwa kuwa simu ni kifaa muhimu kwa mawasiliano na pia kupata taarifa mbalimbali hasa katika kipindi hiki ambacho dunia imekumbwa na janga la Covid-19.

"Taarifa za namna ya kujikinga na maambukizo zinatumwa na hivyo walengwa wanakuwa na uelewa na pia kama kuna taarifa yoyote kuhusu malipo wanaweza kuipokea moja kwa moja kwenye simu zao," alisema Mwamanga.

Hata hivyo, alisema, katika kipindi hichi Tasaf itahudumia kaya za walengwa 1,800,000 katika halmashauri zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

# Ufuta kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani

**Na Mwandishi Wetu, KONDOA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameziagiza halmashauri zote za mkoani humo kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye zao la ufuta ili kulinda maslahi ya mkulima.

Kauli hiyo aliitoa jana akiwa katika ziara yake ya kikazi wilayani Kondoa.

Alisema kila uongozi wa halmashauri unatakiwa kuhakikisha unadhibiti vyema mfumo huo ili kufanya kazi bila ya kuwapo na malalamiko yoyote.

Alitaka vipimo vidhibitiwe ili mkulima kuwa na amani katika bidhaa yake kwa kupita kwenye minzani ambayo ni sahihi.

"Kuna haja ya kuongeza vituo vya ukusanyaji ufuta ili kumpunguzia mkulima umbali wa kusafirisha mazao yake, pia wafanyabiashara wadogo ngazi ya kijiji wanaweza kuuziana wenyewe mazao ili kuweza kujipatia fedha ya mahitaji muhimu na atakayenunua lazima apitishe mazao hayo kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani," alisisitiza.

Aidha, alisema kiwango cha kununua kwa mkulima kisiwe zaidi ya kilo 100, kwa kuwa zaidi ya kiwango hicho mkulima anatakiwa kwenda kuuza katika mfumo rasmi wa stakabadhi ghalani.

Mkuu huyo alisema kuwa ufuta utakaokusanywa utapelekwa kwenye mfumo rasmi, ili mkulima kupata stahiki zake na atalipwa ndani ya siku 10 baada ya mnada.

"Natoa wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Dodoma kufungua benki akaunti ili kurahisisha malipo yenu katika ulipwaji," alisema.

Mahenge alitaka kila halmashauri kuendelea kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa wananchi kuanzisha vyama vya ushirika na masoko ya ndani ya vijiji kwa lengo la kuwasogezea huduma wananchi wanao wahudumia.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, alisema kuwa mazao ya choroko, dengu, mbaazi na ufuta yatauzwa katika mfumo wa stakabadhi ghalani kwa lengo la kumkomboa mkulima kufikia malengo yake na kujiendeleza katika kilimo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) Pabui, Juma Hussein, alisema kuwa wao wanajukumu kubwa la kutafuta masoko ili kuuza mazao hayo ya wakulima na kuhakikisha wanapata stahiki zao bila kukandamizwa.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo (kulia), akinawa maji na sabuni kwenye vifaa vya mfumo wa kunawa mikono vilivyotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), baada ya kuvikabidhi kwa uongozi wa Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NEC yaombwa mazingira rafiki kwa wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetakiwa kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu wakati wa kuandikisha watu katika daftari la kudumu la mpigakura.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu, (Hope Delivery Foundation), Michael Salali, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na kero mbalimbali wanapofika sehemu za kujiandikisha, ikiwamo kutokuwa na alama za nundu kwa ajili ya watu wasioona.

Pia alisema walemavu wa miguu wanalazimika kuwa na wasaidizi kwenye kupanda ngazi kutokana na kukosekana kwa mazingira rafiki kwa ajili yao.

"Changamoto hizo zimesababisha baadhi yao kushindwa kutimiza jukumu lao kikatiba la kuboresha taarifa zao au kujiandikishia katika daftari la mpigakura, lakini wapo waliofanikiwa kwenda, lakini walilazimika kuwa na wasaidizi maana unakuta sehemu wanapoandikishia kuna ngazi hakuna barabara ya watu wenye ulemavu," alisema.

Alisema tume hiyo ina wajibu wa kuhakikisha kuna mazingira rafiki kuanzia unandikishaji hadi upigaji kura.

Katika hatua nyingine, Salali alisema shirika limejipanga kutoa msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona kwa watu wasio na uwezo.

Alisema msaada huo utaambatana na utoaji wa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizo hayo ili kuungana na serikali katika kupambana na ugonjwa huo.

Aliwataka wadau wengine kila mmoja kwa nafasi yake kuendelea kutoa elimu kwa mtu mmoja mmoja pamoja na kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo.

Naye, mmoja wa wakazi wa Dodoma, Simon Joseph, alisema kama serikali haikuweka mazingira rafiki kwa watu wa aina hiyo inawakosesha haki yao ya kuboresha taarifa zao pamoja na kujiandikisha.

Alishauri kuwa ni vyema maandalizi yakafanyika mapema kwa ajili ya watu hao ili kutokumbana na kero wakati wanapofika kwenye vituo vya kujiandikishia.





## Wabeba mizigo wachangia saruji ujenzi wa shule

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

KIKUNDI cha vijana wabeba mizigo wa Kijiji cha Kapunga, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wametoa msaada wa mifuko 20 ya saruji kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa shule mbili za sekondari unaoendelea katika Kata ya Itamboleo.

Wakizungumza jana wakati wa kukabidhi mifuko hiyo kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Itamboleo, Rashid Ngavano, walisema kauli ya Rais John Magufuli ya kuwataka kuchapa kazi hata katika kipindi cha janga la corona imewasaidia kujiingizia kipato na ndipo wakaamua na wao kuchangia maendeleo kwenye jamii.

Mmoja wa wanakikundi hao, Lusajo Mwanyonga, alisema wanatambua jitihada zinazofanywa na serikali, hivyo kwa kuunga mkono walichangisha fedha na kununua saruji mifuko 20, ili isaidie kwenye ujenzi unaoendelea.

"Tunamshukuru Rais wetu kwani amekuwa mstari wa mbele kutuhamasisha tuendelea kuchapa kazi licha ya janga hili la corona... sisi makuli wa mizigo ambao tunabeba magunia ya mipunga kupeleka kwenye malori tumeamua kusaidia sekta ya elimu ili watoto na wadogo zetu wapate elimu kwenye mazingira mazuri," alisema Mwanyonga.

Mratibu Elimu wa Itamboleo, Upendo Shimwela, alikishukuru kikundi cha vijana hao kwa msaada walioutoa na kuwaomba wengine kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea.

Diwani wa Itamboleo, Lwitiko Mwangosi, alisema kuwa hiyo ndiyo faida ya malezi bora kwa vijana, na kwamba msaada huo utakuwa chachu ya kumaliza kero wanayoipata wanafunzi kutembea umbali wa kilometa 13 kwenda shule.

# Majitaka yawaondoa wapangaji wa NHC

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwaondoa wapangaji wote katika jengo la Cinema lililopo katikati ya Jiji.

Uamuzi huo umetokana na shirika kushindwa kuweka miundombinu ya majitaka, hali inayosababisha maji machafu kutiririka ovyo mitaani na kuhatarisha afya za wananchi.

Jengo la cinema lenye ghorofa moja ambalo ni mali ya shirika hilo lipo mtaa wa Lupa, mkabala na Posta, katikati ya Jiji la Mbeya, lina wapangaji zaidi ya 15, lakini halina mfumo wa majitaka.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa Afya wa Kata ya Sisimba, John Oden, alisema aliamua kuchukua hatua ya kuwahamisha wapangaji hao kwa lengo la kunusuru afya zao.

Alisema uamuzi huo uko kwa mujibu wa sheria na kwamba anachokifanya sasa ni kuandika notisi ya kuwaondoa wapangaji wote hadi hapo atakaporekebisha mfumo wa majitaka.

Hata hivyo, baadhi ya watumiaji wa jengo hilo, walisema kukosekana kwa miundombinu ya majitaka imekuwa ni hatari kwao kutokana na harufu mbaya.

Mmoja wa wapangaji hao, Brighton Ngowi, alisema jengo hilo ambalo wanalitumia kibiashara, limekuwa likisababisha kero kwa wateja na wananchi wengine kutokana na hafuru inayosikika.

Akizungumzia kadhia hiyo, Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Mbeya, Said Bundala, alisema wameshachukua hatua kwa kulipia gharama za uwekaji wa mfumo wa majitaka katika jengo hilo.

Alisema zaidi kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani humo, ndiyo inayosuasua kufanya kazi hiyo, huku mkuu wa kitengo cha mfumo wa majitaka wa mamlaka hiyo, Mhandisi Yasin Msuya, akieleza changamoto zinazokwamisha kazi hiyo kufanyika kuwa ni wananchi kuendeleza shughuli za ujenzi kwenye maeneo ambayo yanahitaji huduma za kijamii.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akifanya ukaguzi wa uvaaji wa barakoa kwa abiria kwenye vyombo vya usafiri katika stendi ya Kabwe, jijini Mbeya juzi, kwa ajili ya kijikinga na maambukizo ya corona. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Familia yaiangukia serikali uchunguzi kifo cha ndugu yao

**Na Graace Mwakalinga, MBEYA**

FAMILIA ya Konga, wakazi wa Kata ya Chimala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, imeiomba serikali kufanya uchunguzi kuhusu chanzo cha kifo cha mtoto wao, Tulizo Konga(38) kilichotokea Machi 25, mwaka huu akiwa nyumbani kwake.

Kwa mujibu wa maelezo ya wanafamilia hao, mtoto wao alifariki ghafla akiwa mikononi mwa familia alikokuwa ameolewa.

Utata wa kifo hicho ulianza baada ya upande wa familia ya marehemu kudai kuwa hawakupewa taarifa ya kifo cha mtoto wao mpaka pale walivyopata taarifa za kifo hicho kupitia majirani.

Akizungumza na Nipashe, kaka wa marehemu, Msafiri Konga, alisema hadi wanaenda kuzika walikataliwa kuuona mwili.

Konga alisema kifo cha dada yao kimeibua sintofahamu kutokana na kutopata taarifa yoyote tangu afariki na kwamba wamezunguka kwa mkuu wa upelelezi wilaya kwa mwezi mmoja bila kupewa majibu.

"Nilipigiwa simu kuhusu kifo cha ndugu yangu na majirani wakati aliolewa sijui kuna kitu gani nyuma ya pazia, lakini tulitarajia kuona mwili wa marehemu," alisema Konga.


Mdogo wa marehemu, Fadhil Konga, aliiomba serikali pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na familia kutambua aliyezikwa kama kweli ndugu yao na chanzo chake cha kifo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Posta, Edward Mkuti, alisema kifo cha Tulizo kina utata kwani siku moja kabla ya mauti alikuwa mzima wa afya akiendelea na shughuli zake za kuuza duka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema kifo kilitokana na ugonjwa aliokuwa nao wa uvimbe kichwani.

Alisema kifo chake kiligundulika na mtoto wa marehemu akiwa amelala baada ya kujiuma ulimi mara mbili.

Kwa mujibu wa taarifa za Hospitali ya Misheni ya Chimala, marehemu alifikishwa hospitalini hapo akiwa amefariki dunia, hivyo hawakuweza kufanya uchunguzi wowote zaidi ya kutoa kibali cha mazishi.





# Rais Shein kuhutubia Baraza la Eid kimtandao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imesema sherehe za Baraza la Eid hazitafanyika katika mfumo uliozoeleka wa waumini wa dini ya Kiislamu kukusanyika na kufanya sala ya pamoja ya kitaifa.

Katibu wa Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Khalid Ali Mfaume, akizungumza na waandishi wa habari alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, anatarajiwa kulihutubia Baraza la Eid kupitia vyombo vya habari siku ya Iddi.

Alisema hatua hizo ni kwa ajili ya kuchukua tahadhari ya kupambana na ugonjwa wa Covid-19 na kupunguza mikusanyiko inayoweza kusababisha maambukizo mapya.

"Tulikuwa tumezoea Baraza la Eid waumini wanakusanyika pamoja na Rais wa Zanzibar kutoa hotuba yenye mnasaba wa sherehe hizo na kupata vinywaji...mwaka huu kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa corona tumebadilisha mfumo na Rais atazungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari," alisema.

Shekhe Mfaume alisema ibada ya sala ya Eid zitafanyika kupitia katika misikiti ya waumini mbalimbali maeneo yao na hakutakuwa na sala ya pamoja ya kitaifa.

Alizitaka kamati za misikiti kuhakikisha kwamba zinafuata masharti ya kujikinga na ugonjwa wa corona ikiwamo kufupisha ibada hizo pamoja na hotuba.

Pia, aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu kuhakikisha wakati wa kufanya ibada wanaweka masafa ya mita moja na nusu ikiwa ni tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Ofisi ya Mufti imeweka utaratibu mzuri wa kufanya ibada katika misikiti mbalimbali na waumini wanaombwa kuzifuata ili ibada ziwe salama zaidi," alisema Mfaume.

Waumini wa dini ya Kiislamu nchini na duniani kote wanatarajiwa kuanza kusherehekea Sikukuu ya Eid kuanzia Jumapili au Jumatatu baada ya kuonekana kwa mwezi wakihitimisha kumalizika kwa mfungo wa mwezi wa Ramadhani ambao ni miongoni mwa nguzo tano za dini hiyo.

# Vikundi kunufaika mikopo ya mil. 850/-

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MFUKO wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umejipanga kutoa mikopo 700 yenye thamani ya Sh. 850,000,000 kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali Unguja na Pemba ili kujikomboa na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Hayo yalisemwa na Kaimu Waziri wa Uwezeshaji Wanawake na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021, katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Unguja.

Pembe alisema miongoni mwa mikakati inayotarajiwa kuchukuliwa na mfuko huo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa vikundi ambavyo vitapata mikopo hiyo ili miradi yao iwe endelevu na kuleta tija kwa walengwa.

Alisema ili kuhakikisha mikopo inayotolewa inatumika ipasavyo, watahakikisha wanafuatilia watu wote waliopewa mikopo hiyo pamoja na kuwapatia mafunzo.

"Wizara kwa mwaka wa fedha 2020-2021 imejipanga kuwawezesha wajasiriamali pamoja na vikundi vya Saccos na vyama vya ushirika ili wanachama wake waweze kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020-2021, wamejipanga kuhakikisha vyama vya ushirika vinapiga hatua kubwa na tayari jumla ya vyama vya ushirika 186 vimesajiliwa kati ya hivyo 104, Pemba na 82 Unguja.

Kwa upande wa vyama vya ushirika alisema wananchi wamehamasika kujiunga huku wanawake wakionyesha mwamko mkubwa katika vikundi vya kuweka na kukopa.

Alisema kwa upande wa vyama vya ushirika wamejipanga kutoa elimu ya uendeshaji wake wenye tija pamoja na ukaguzi wa vitabu vya mahesabu na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Riziki aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. 18,510,451,000 kwa mwaka wa fedha 2020-2021, kati ya hizo Sh. 15,251,300,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Sh. 10,095,200,000 kwa matumizi ya uendeshaji wa programu za wizara pamoja na matumizi ya mishahara.



Meneja Mauzo wa TBL Plc, Peter Mweta (wa pili kulia), akimkabidhi Mmiliki wa Baa ya New Joint iliyopo External Ubungo, Olvari Shirima (katikati), msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19, uliotolewa na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya wahudumu na wateja ikiwa ni mwendelezo wa TBL, kuunga mkono jitihada za serikali za kupambana na maambukizo ya ugonjwa huo. Baa zaidi ya 2,500 nchini kupatiwa msaada huo. Kushoto ni Ofisa wa Ukuzaji Masoko wa TBL, Neema Mkama na wafanyakazi wa baa hiyo, Felista Patilio na Josephine Mshama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Z'bar yajipanga utalii kuimarika Pemba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kuhakikisha sekta ya utalii inaimarika katika kisiwa cha Pemba na kukuza uchumi wa taifa na pato la wananchi kwa ujumla.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema tayari serikali imetangaza utalii kwa wote kwa lengo la kuwanufaisha wananchi na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Alisema serikali inakusudia kuliimarisha eneo la Kaskazini ya Micheweni kuwa moja ya kivutio cha watalii kwa kujenga hoteli kubwa za kitalii.

Alikiri kuwa sekta ya utalii imechelewa kuimarika katika kisiwa hicho kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa miundombinu ya umeme na barabara.

"Tunawataka wananchi wa kisiwa cha Pemba kujipanga na kujitayarisha kupokea utalii ambao miongoni mwa faida zake kubwa ni kukuza pato la wananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisema. Vile vile, Kombo alikemea na kuwataka wananchi kuacha kuuza maeneo yao ya vijijini ikiwamo yaliopo pembezoni mwa fukwe za bahari kwa wawekezaji na watu wanaotaka kumiliki maeneo hayo kwa shughuli za utalii.

Alisema njia nzuri na ushauri wa serikali ni kuingia ubia na watu wanaoyataka maeneo hayo kwa ajili ya kujenga hoteli za kitalii na mradi huo utaendeshwa kwa njia ya ubia. "Ukiingia ubia katika jengo la hoteli iliyojengwa maana yake wewe utafaidika na hisa iliopo pale katika muda wote wa maisha yako na ukifa itafaidika familia yako hadi watoto," alisema.

Baadhi ya wananchi waliochangia bajeti hiyo waliitaka serikali kuhakikisha kwamba utalii unadumisha utamaduni na silka za wananchi.

Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahani, alisema wananchi wa Pemba wapo tayari kuupokea utalii baada ya kuimarika kwa miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara na umeme hadi vijijini.

"Wananchi wa Pemba wanaisubiri serikali na sekta binafsi kufungua milango ya sekta ya utalii kwa ujenzi wa miradi ya hoteli ili wananchi wafaidike kwa kuuza bidhaa zao mbalimbali na kupata fedha," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa jumla ya Sh. 20,389,800,000, kati ya hizo Sh. 14,289,800,000 kwa kazi za kawaida na Sh. 6,100,000,000 kwa kazi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**Anahitajika Boharia au (Store Keeper) na Muuguzi Msaidizi au (N/A)** Kwa anayehitaji apige simu namba: 0786 641 903/ 0716 172929


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi No;121/2020

Ombi la MANENO HAMIS KIBODE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HAMIS RAMADHANI KIBODE .**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/05/2020

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

157465

**KUPOTEA KWA PASIPOTI/HATI YA KUSAFIRIA**



Noel Odeny Chacha anatangaza kupotea kwa Passport/Hati ya kusafiria yenye namba AB192205 iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2006.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/KIJ/RB/232565/2020

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Asanterabi Samson Massam** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1284.0043.2010** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika Shule ya Sekondari Northen Highlands.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/451786/2019**

157459

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**SHAURI NA 86 LA 2019**
**MAWENI LIMESTONE LTD………………..MDAI**
**DHIDI YA**
**FRANCIS THEOPIL NGOWI NA WENGINE 9**
**….WADAIWA**

**KWA: LUVI JOHN PATRIC, GODFREY JOHN PATRIC, AMIRI MJATA, MAGETA STANLEY, GERAD ALEX MALIGA, OMARY MJATA – POPOTE MLIPO.**

Mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Unaarifiwa kufika mnamo tarehe 21/5/2020 saa tano (05:00) asubuhi ambapo shauri hili litakuja kutajwa. Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri/lakiri ya Baraza hili leo tarehe 18 Mei, 2020.

MWENYEKITI
TANGA

157461


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mitandao ya kijamii Burundi yazimwa uchaguzi

**BUNJUMBURA,** Burundi

MITANDAO ya kijamii nchini Burundi siku ya jana ilizimwa wakati wananchi wakiendelea kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu.

BBC ilithibitisha kuwa mitandao ya Twitter, WhatsApp na Facebook ilikuwa haipatikani nchini lakini Serikali haikulizungumzia suala hilo.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa kutoka saa 12 asubuhi na vilitarajiwa kufungwa saa 10 alasiri.

Wagombea saba wanawania kumrithi Pierre Nkurunziza, lakini kati yao wawili ndiyo wanaopigiwa upatu zaidi, kutoka chama cha upinzani CNL, Agathon Rwasa na chama tawala CNDD-FDD, Evariste Ndayishimiye.

Raia wa Burundi wanapiga kura ya kumchagua rais, na katika karatasi za kupigia kura, jina la Nkurunziza halipo.

Siku ya jana ilikamilisha utawala wa Nkurunziza ambaye aliingia madarakani katika taifa hilo la Afrika Mashariki miaka 15 iliyopita.

Uchaguzi huo pia unahusisha nafasi za ubunge na madiwani na matokeo yake yanatarajiwa kuanzia kutolewa Mei 25. **BBC**



Wagombea saba wanaowania nafasi ya urais nchini Burundi ya kumrithi Pierre Nkurunziza. **PICHA: MTANDAO**

# Trump ajisifu idadi kubwa maambukizo

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS Donald Trump amesema ni heshima kwa Marekani kuwa na idadi kubwa ya maambukizo ya virusi vya corona duniani.

"Ninalitazama suala hili kama heshima fulani, kama jambo zuri kwa sababu inamaanisha kuwa vipimo vyetu viko vizuri," Rais Trump aeleza akiwa Ikulu.

Marekani ina watu milioni 1.5 walioathiriwa na virusi vya corona na karibu vifo 92,000, kwa mujibu wa takwimu zinazokusanywa na Chuo Kikuu cha Johns Hopkins.

Nchi inayoshika nafasi ya pili ni Urusi ikiwa na maambukizi ya watu 300,000.

Siku ya Jumatatu, Trump alikuwa akihodhi mkutano wake wa kwanza wa baraza la mawaziri tangu kuanza kwa mlipuko wa virusi hivyo nchini Marekani.

Aliwaambia waandishi wa habari, "Unajua unaposema kuwa tunaongoza kuwa na watu wengi walioambukizwa, ni kwa sababu tuna vipimo vingi kuliko mtu mwingine yeyote."

"Hivyo tuna watu wengi walioambukizwa, sitazami kama jambo baya, ninalitizama kwa heshima fulani, kama jambo jema kwa sababu ina maanisha kuwa tuna vipimo vizuri.

Kwa mujibu wa kituo cha kupambana na kudhibiti magonjwa, Marekani imepima watu milioni 12.6 mpaka siku ya Jumanne.

Trump alikuwa akijibu swali kuhusu kama alikuwa akifikiria kuweka marufuku ya kusafiri kwenda Amerika ya Kusini hasa Brazil. Nchi hiyo ni ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya waathirika wa virusi vya corona, ikiifuata Marekani na Urusi.

Kamati ya uongozi ya kitaifa ya chama cha Democratic imekosoa kauli ya Trump, ikisema kwenye ukurasa wake wa Twitter kuwa na waathirika wa corona milioni 1.5 nchini Marekani kunaonesha kushindwa kabisa kwa uongozi. **BBC**

## Vifo corona Brazil vyafikia 1,000

**BRASILIA,** Brazil

BRAZIL imerekodi vifo 1,179 vya corona katika kipindi cha masaa 24 yaliyopita jana.

Hii ni mara ya kwanza kwa idadi ya vifo ya siku moja kufikia 1,000.

Kulingana na wizara ya afya nchini humo, idadi ya vifo imefikia 17,971. Maambukizo mapya katika muda kama huo yalifikia 17,408 na jumla ya watu 271,628 wameambukizwa.

Wataalamu wa afya ya umma walisema kiwango cha juu kabisa kinatarajiwa kufikia mwanzoni mwa mwezi Juni, na kuongeza kuwa takwimu za serikali kwa kiasi kikubwa huenda hazitoi uhalisia wa vifo na maambukizo kwa kuwa Brazil inafanya vipimo vichache vya corona. **DW**

## WHO kukabiliwa na uchunguzi

**GENEVA, Uswizi**

SHIRIKA la Afya Ulimwenguni, (WHO) limekubali kuanzisha uchunguzi wa namna lilivyoushughulikia mzozo wa virusi vya corona.

Uchunguzi huo unakuja wakati ambapo China inaituhumu Washington kwa kukwepa wajibu wake, baada ya Rais Donald Trump kutishia kujiengua kwenye shirika hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Gebreyuses alisema mapambano ya janga hilo ni lazima yapewe kipaumbele, ingawa ugonjwa huo unaendelea kusababisha vifo na kudhoofisha uchumi kote ulimwenguni.

Rais Trump ameituhumu WHO kuwa ni kibaraka wa China na limeshindwa kufanya vya kutosha kukabiliana na kusambaa kwa virusi hivyo.

Siku ya Jumatatu, Trump alitishia kuondoa kwa muda ama moja kwa moja ufadhili wa Marekani kwenye shirika hilo na Beijing ilijibu kitisho hicho jana, kwa kumtuhumu Trump kujaribu kuichafua China na kuivuruga WHO kwa manufaa ya kisiasa. **DW**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM.**

**COMMERCIAL CASE NO. 32 OF 2019**

**STANDARD CHARTERED BANK**
**TANZANIA LIMITED................................PLAINTIFF/APPLICANT**

**VERSUS**

**TESTA LIMITED ............................1ST DEFENDANT/RESPONDENT**
**JOHN JOHN MNYIKA ...................2ND DEFENDANT/RESPONDENT**
**LAZARO OBADIA MTANI...............3RD DEFENDANT/RESPONDENT**

**DECREE**

**WHEREFORE,** the Plaintiff lodged this case against the defendants praying for judgment and decree as follows:-

i. Payment of the sum of Tanzania Shillings Two Hundred Fifty Nine Million Nine Hundred Sixty Forty Thousand Nine Hundred Ninety Cents Ninety eight (TZS 259,964,990.98) as of 22nd January 2019 being the outstanding amount on account of the Credit Facility.
ii. Interest on the outstanding amount specified at (i) above at the rate of Twenty three percent (23%) from 22nd January 2019 to the date of judgment.
iii. Interest on the decretal amount at the court's rate of seven percent (7%) from the date of judgment until full and final payment.
iv. Costs of the suit
v. Any other reliefs which this honourable court may deem just to grant in favour of the plaintiff.

This matter coming for judgement on this 12th day of May 2020 before Hon. B.K Phillip, Judge in the presence of Advocate Gaspar Nyika for the Plaintiff and Advocate Jeston Justine for the 2nd Defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT:**

i. The 1st and 3rd defendants shall jointly and severally pay the plaintiff the sum of Tanzania Shillings Two Hundred Fifty Nine Million Nine Hundred Sixty Forty Thousand Nine Hundred Ninety Cents Ninety eight (TZS. 259,964,990.98) being the outstanding amount on account of the Credit Facility as at 22nd January 2019.
ii. The 1st and 3rd defendants shall jointly and severally pay interest on the decretal sum in (i) above at the rate of Twenty Three percent (23%) from 22nd January 2019 to the date of judgment.
iii. The 1st and 3rd defendants shall jointly and severally pay interest on the decretal amount at the rate of seven percent (7%) from the date of judgment until full and final payment.
iv. The 1st and 3rd defendants shall bear the costs of the suit.

Given under my hand and seal of the court on this 12th day of May 2020.

THE HIGH COURT OF TANZANIA COMMERCIAL DIVISION

**B.K. PHILLIP**
**JUDGE**

Extracted on this 18th day of May 2020.

xxxxxx

# HATIMA YA CITY UEFA JUNI 10



**PARIS,** Ufaransa

MAHAKAMA ya Usuluhishi wa Michezo (CAS), imesema kuwa rufaa ya klabu ya Manchester City, itasikilizwa Juni 8 hadi 10 na kutoa hukumu.

Manchester City waliwasilisha rufaa mahakamani hapo kupinga adhabu iliyotolewa na Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), baada ya kukutwa na kosa la kukiuka kanuni za matumizi ya kiwango cha fedha za usajili.

Timu zote Ulaya zimewekewa kiwango cha juu wanachoruhusiwa kutumia katika kusajili ili kuzipa nafasi sawa timu zisizo tajiri kuweza kushindana kwa usawa ingawa hazina utajiri wa kutisha.

Kama klabu hiyo itaendelea kuthibitika ina kosa la kukiuka kanuni za matumizi ya kiwango cha fedha za usajili, haitoshiriki michuano hiyo kwa muda wa miaka miwili na nafasi yao itachukuliwa na timu itakayomaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Adhabu ya awali inaifanya Manchester City kutoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Barani Ulaya, Ligi ya Europa katika misimu miwili ya 2020-2021 na 2021-2022 na faini ya euro milioni 20.

# Majaliwa ya Coutinho hayajulikani

**MUNICH,** Ujerumani

MAJALIWA ya Philippe Coutinho bado hayajulikani licha ya raia huyo wa Brazil muda wake wa kucheza kwa mkopo pale Bayern Munich kuelekea mwishoni, kwa mujibu wa wakala wake, Kia Joorabchian.

Coutinho mwenye umri wa miaka 27, alijiunga na Bayern kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua Agosti, mwaka jana baada ya kuwa na msimu usio na mafanikio kule Camp Nou, awali akiwa amecheza Liverpool.

Kiungo huyo ameshindwa kutamba kule Ujerumani akifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi 22 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na Bayern imeripotiwa kwamba haina mpango wa kumnunua moja kwa moja kwa ada yake inayotajwa kuwa ni euro milioni 120.

Nyota wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz na mkali wa Manchester City, Leroy Sane ametajwa kuwa kwenye orodha ya kuwindwa na Bayern Munich na hivyo nyota huyo kuonekana kutokuwa na muhimu kwa miamba hao wa Ujerumani.

"Naweza kusema kwamba Philippe ana furaha kubwa hapa Munich," alisema Joorabchian akiiambia Sport1.

"Anaipenda klabu na ana malengo makubwa ya kutaka kuendelea kubakia kwenye timu hii.





# *Marseille yampa ofa Villas-Boas*

**PARIS,** Ufaransa

ANDRE Villas-Boas amepewa ofa ya miaka miwili ya kuendelea kuinoa klabu ya Marseille wakati uvumi ukienea kuhusu majaliwa ya raia huyo wa Ureno.

Kocha wa zamani wa Porto, Chelsea na Tottenham, Villas-Boas alikuwa na msimu wa kuvutia baada ya kuchukua mikoba kutoka kwa Rudi Garcia pale kwenye dimba la Velodrome Mei, mwaka jana na kuiwezesha Marseille kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa, 2019-20.

Mwanzoni mwa mwezi huu, kocha huyo mwenye umri wa miaka 42 alibainisha kwamba majaliwa yake ya kubakia kwenye timu hiyo ni kama atatimiziwa mahitaji yake hasa kwenye suala la usajili wa wachezaji.

RMC Sport iliripoti Jumanne kwamba, Villas-Boas alikataa ofa ya kuongezea mkataba wa mwaka mmoja, ambapo wa sasa unamalizika Juni 2021.

Hata hivyo, Marseille ilitoa taarifa ya kufafanua walikuwa wakisubiri majibu ya ofa yao kutoka kwa kocha huyo na wanataka kumwongezea miaka miwili zaidi.

"Baada ya habari kutoka kwenye vyombo vya habari kuhusu kuongeza mkataba kwa kocha Andre Villas-Boas, Olympique de Marseille ingependa kutoa ukweli halisi," ilisomeka taarifa ya klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO




# LIVERPOOL YAJIPANGA KUMTULIZA MANE

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imepanga kuhakikisha inambakisha nyota wao, Sadio Mane ili asichukuliwe na Real Madrid wanaotajwa kumwania katika dirisha lijalo la usajili.

Mchezaji huyo raia wa Senegal amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho 12 katika mechi alizocheza na kuisogeza Liverpool karibu na ubingwa wa Ligi Kuu England (EPL).

Ubora na kiwango chake cha uwanjani kimemfanya hata kuchaguliwa kushika namba nne kwenye tuzo za Ballon d'Or za mwaka jana.

Mshambuliaji huyo alisajiliwa kwa mkataba wa miaka mitano kuchezea timu hiyo ya Anfield, Novemba 2018.

Licha ya hilo, kumekuwa na mazungumzo ya kumhusisha mchezaji huyo kwenda Bernabeu huko Madrid ili akaichezee timu hiyo.

Kwa mujibu wa Football Insider, Liverpool ipo tayari kumpa Mane dili tamu ili kumfanya aendelee kubaki kwenye kikosi hicho cha mabingwa watarajiwa wa Ligi Kuu England.

## Aston Villa kutoshusha bei ya Grealish

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imeweka bayana kwamba haina mpango na wala haifikirii kabisa kushusha bei ya supastaa wao, Jack Grealish, ataendelea kuuzwa pauni milioni 80 hata kama watashuka daraja.

Kiungo huyo mshambuliaji, Grealish mwenye umri wa miaka 24, amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu katika kikosi hicho cha Kocha, Dean Smith akifunga mara tisa na kuasisti mara nane katika mechi 31 alizocheza kwenye michuano yote.

Aston Villa inashika nafasi ya 19 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na watakuwa kwenye vita kali ya kukwepa kushuka daraja wakati ligi itakaporejea wiki chache zijazo. Manchester United imekuwa ikihusishwa na mchezaji huyo na imeripotiwa kuwa na matumaini kwamba thamani yake itashuka na kufika Pauni 50 milioni kama Aston Villa itashuka daraja.

Hata hivyo, kwa mujibu wa The Mirror, Aston Villa hawatashusha thamani yake na kwamba wataendelea kumuuza kwa dau lile lile.







## Raktic afunguka kuondoka Barca

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Ivan Rakitic amebainisha kuwa, anafikiria kuondoka na kutafuta timu nyingine, katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Mkataba wa sasa wa Rakitic unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu ujao na Barcelona wameripotiwa kuwa tayari kumuuza katika dirisha lijalo la majira ya joto, ili kuepuka asiondoke bure pindi mkataba wake utakapomalizika mwakani.

Tetesi zinadai kuwa Rakitic anawaniwa na klabu mbalimbali kama vile Atletico Madrid, Napoli, Villarreal, Juventus, Sevilla, Manchester United na Tottenham.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye tangu ajiunge na Barcelona mwaka 2014, amefanikiwa kushinda mataji 13 alisema anadhani sasa ni wakati wa kusaka maisha kwingine badala ya kuendelea kubakia Barcelona.

"Mchezaji anaposaini mkataba na klabu fulani, lazima atimize vile vipengele kwenye mkataba huo," alisema akinukuliwa na gazeti la AS.

"Shauku yangu mimi ni kuhitaji kucheza jambo ambalo linanifanya nitafute sehemu nitakayopata nafasi hiyo.

"Nilihitaji mtu kutoka Barcelona aje na kusema hadharani kwamba bado wana nihitaji na nitaendelea kubaki klabuni hapo mpaka mwisho wa mkataba wangu, lakini hilo silioni jambo linalofanya niwe tayari kuitumikia timu yeyote itakayohitaji saini yangu," alisema.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ROSE AMPELEKA POCHETTINO UTD

**Anaamini uwezo wa kocha huyo wa zamani wa Spurs ni wa kufundisha klabu kubwa...**

**LONDON,** England

DANNY Rose amesema kocha wake wa zamani na Tottenham, Mauricio Pochettino, anaweza kumalizia kazi yake ya kufundisha soka katika klabu kubwa na hana wasiwasi na hilo na anaona ana nafasi ya kutua kwenye kikosi cha Manchester United.

**Kocha huyo raia wa Argentina alifukuzwa Tottenham Novemba mwaka jana huku timu hiyo ikiwa inapambana katikati ya msimamo wa Ligi Kuu England, ikiwa ni mwezi mmoja tangu afungwe mabao 2-0 kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool iliyochezwa jijini Madrid.**

Akiwa na klabu hiyo ya London Kaskazini, Pochettino alikuwa karibu na wachezaji wake nyota wa akiwamo Rose, na beki huyo wa kushoto ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Newcastle, anafikiria kocha huyo bado ana nafasi nzuri ya kwenye kazi yake.

Alipoulizwa wakati huu wa kufanya mazoezi katika kipindi cha kukaa nyumbani kuhusiana na hatima ya Pochettino kupata klabu kubwa ya kufundisha, Rose alisema: " Bila ya shaka yoyote, kwa kufahamu uadilifu wake ambao aliupata pia kutoka [Marcelo] Bielsa. Ninajua Poch, ambaye ana asili ya Bielsa. Watu wengi wamepata kukua na kuimarika kutoka kwenye mikono yake."

Na alipouliwa ni timu gani anadhani kocha huyo anaweza kujiunga nayo, beki huyo aliongeza: 'Itakuwa United.'

Kwa muda mrefu Pochettino amekuwa akihusishwa na tetesi za kujiunga na Manchester United hasa pale Ole Gunnar Solskjaer alipokuwa na wakati mgumu kwenye kikosi hicho cha Old Trafford.

Kwa siku za hivi karibuni, kocha huyo amekuwa akitajwa kuenda akajiunga na Newcastle baada ya wamiliki wapya kutoka Saudi Arabia watakapokamilisha mchakato wa kuimiliki klabu hiyo, na pia aliwahi kutajwa kutakiwa na Real Madrid.

Rose anamwona Pochettino ni moja ya makocha wenye uwezo wa juu baada ya kufanikiwa kutengeneza kikosi cha kwanza imara mara tu alipojiunga na Spurs Mei mwaka 2014.

Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England ambaye ana umri wa miaka 29, alisema kocha huyo wa zamani wa Southampton amemtaka kuendelea kufuata misingi ya uchezaji na anaamini ataendelea kuimarika, na amemwahidi atafanya hivyo ili aweze kupata nafasi ya kucheza kila mara kwenye kikosi cha Three Lions.

Kwa sasa amekuwa mbali na kiwango alichokionyesha wakati wanaifunga Ajax kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kueleza kuwa Pochettino alilazimika kuwaruhusu wachezaji wa Spurs kusheherekea ushindi huo usiku tofauti na tamaduni ya klabu hiyo.

"Chini ya Poch, alikuwa na utamaduni tofauti na wa Waingereza. Haikuwa hivyo, hakuwa anawaelewa, unajua Waingereza wanapenda kunywa, ni jambo ambalo kwake halikuwa la kawaida."

## ZISIKUPITE

### SANE AIKATAA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Leroy Sane, amesema hayuko tayari kujiunga na mahasimu wao katika Ligi Kuu England, Liverpool. Nyota huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 24 anajiandaa kutua Bayern Munich.***(Bild, via Sports Illustrated)***

### HAALAND ATOBOA SIRI

STRAIKA wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland (19), alikataa kujiunga na Juventus kwa sababu mabingwa hao wa Italia walitaka kumweka nyota huyo raia wa Norway kwenye kikosi cha Timu ya vijana wa umri chini ya miaka 23 (U-23). ***(La Repubblica, via Star)***

### UNITED YAMTAKA TRAORE

MANCHESTER United ni moja ya timu zinazowania saini ya winga wa Wolverhampton Wanderers, Adama Traore (22). Klabu nyingine zilizoko kwenye mbio hizo ni pamoja na Liverpool na Manchester City. ***(Birmingham Mail)***

### DIABY ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inaamini itafanikiwa kumsajili winga wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya vijana ya Ufaransa ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Moussa Diaby. Mfaransa huyo ambaye aliwahi kuitumikia Paris St-Germainalitoa pasi mbili za mwisho wakati Leverkusen ikiwafunga mahasimu wao katika Bundesliga, Werder Bremen Jumatatu iliyopita. ***(Le10Sport - in French)***

### MBUYAMBA KUTUA CHELSEA

CHELSEA inatajwa kuongoza katika mbio za kuwania saini ya beki wa kati wa Uholanzi, Xavier Mbuyamba kutoka kwa vigogo wa Hispania, Barcelona, taarifa ya wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 imesema. ***(Voetbal International, via Mail)***

### VERTONGHEN AGOMBEWA

KLABU mbalimbali za Ulaya zimeonyesha nia ya kumsajili beki wa Spurs, Jan Vertonghen (33), ambaye anamaliza mkataba wake na klabu hiyo katika majira ya joto. Mbelgiji huyo anawaniwa na Real Betis, Valencia za Hispania pamoja na Inter Milan na Roma kutoka Italia. ***(Star)***

### GARNER KUONDOKA UNITED

KIUNGO wa Manchester United, James Garner (19), ataruhusiwa kuondoka na kujiunga kwa mkopo katika klabu nyingine ifikapo msimu ujao. Timu zinazoshiriki Championship ikiwamo Cardiff City, Swansea City na Sheffield Wednesday zinawania saini ya nyota huyo raia wa England. ***(Mail)***

### JUVE KUUZA NYOTA WAKE

KLABU ya Juventus inaweza kuwauza nyota wake akiwamo kiungo wa Bosnia, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 30, na mshambuliaji wa Argentina, Gonzalo Higuain mwenye miaka 32, kipindi cha majira ya joto kinachokuja kama sehemu ya sera mpya ya kuiwezesha klabu hiyo kuendana na athari ya kifedha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Daily Mail)***

### KLABU EPL MGUU SAWA

KLABU za Ligi Kuu England zikiwamo Liverpool, Chelsea, Arsenal, Tottenham Hotspur na Southampton, zimeanza mazoezi ya pamoja ili kujiandaa na ligi hiyo inayotarajiwa kuendelea tena wakati wowote. Nyota wa Chelsea, Callum Hudson-Odio, ambaye alishikiliwa kwa tuhuma za kubaka naye ameshaungana na wenzake baada ya kupata dhamana. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

## Kaseba aendelea kujiweka imara

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA aliyejipatia umaarufu nchini kupitia mchezo wa Kick Boxing, Japhet Kaseba, amesema anaendelea na mazoezi kwa lengo la kuboresha kiwango chake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaseba ambaye aligeuka na kuwa bondia wa ngumi za kulipwa alisema anatambua madhara ya kukaa muda mrefu bila ya kufanya mazoezi.

Kasema alisema katika kipindi hiki ambacho serikali imesimamisha michezo, yeye anaendelea kujiimarisha kwa sababu anataka kulinda kiwango wake kwa kuupa mwili wake mazoezi kama ilivyokuwa zamani.

"Ninakitendea haki kipaji changu kwa kuendelea kufanya mazoezi kila siku, kipindi hiki nakitumia vizuri kujinoa kwa nguvu huku wanamichezo wote tukisubiri tamko la serikali kama michezo itaendelea kuchezwa au la," alisema Kaseba.

Amewataka mabondia wote wa hapa nchini kutobweteka na kuwakumbusha wakifanya hivyo watashusha viwango vyao na kujiweka kwenye hatari ya kuua vipaji walivyonavyo.

" Nimefarijika na kupata matumaini baada ya kusikia serikali inafikiria kurudisha michezo, uamuzi huu umenifurahisha kwa kiasi kikubwa, naamini kila mmoja hakuacha mazoezi," alisema Kaseba.

Alishauri endapo tarehe ya kuanza kwa michezo itatangazwa, wachezaji wote wapimwe kwanza kabla ya kuendelea tena na mashindano.

## Simba Queens yafikiria ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema mikakati yake ni kuona timu hiyo inafanya vizuri katika michezo yake iliyobakia na hatimaye kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake kwa mara ya kwanza msimu huu.

Mgosi ameliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana mikakati aliyonayo ni kuwabadilishia wachezaji wake programu ya mazoezi ili kufidia muda ambao ligi hiyo ilisimama.

Kiungo huyo mshambuliaji wa zamani wa Simba, alisema ligi itakaporejea, timu yake itafanya mazoezi mara mbili kwa siku.

Alisema anahitaji kuleta mabadiliko katika soka la wanawake hivyo anahitaji kikosi chake kifanikishe malengo waliyonayo na kuleta mapinduzi kwenye ligi hiyo ya juu kwa wanawake hapa nchini.

"Malengo yangu ni kuleta mabadiliko katika mpira wa kike, ninahitaji sana msimu huu kuchukuwa ubingwa sababu hiyo nimekuwa karibu kuwafatilia wachezaji wangu katika kipindi hiki cha janga la corona," alisema Mgosi.

Aliongeza ana imani na kikosi chake na hata ligi hiyo ikirejeshwa leo, hana wasiwasi na nyota wake wa Simba Queens.

Simba Queens inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 29 lakini wana michezo miwili mkononi wakati vinara ni JKT Queens ambao wamecheza mechi mbili zaidi.

# MBEYA CITY YAANIKA SIRI KUBORONGA BARA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya City umesema mabadiliko ya kikosi chao pamoja na benchi la ufundi, ndiyo vimesababisha timu hiyo kufanya vibaya katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea ukingoni, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, amesema mabadiliko hayo yaliwafanya waanze upya wakati timu nyingine zinaendelea 'kuvuna pointi' katika mechi mbalimbali za ligi zilizokuwa zinachezwa.

Kimbe alisema msimu huu haukuwa 'mzuri' kwao kwa sababu walianza ligi vibaya na mabadiliko yaliyofanyika yalichangia kushindwa kuonyesha ushindani.

**Alisema kuondoka kwa wachezaji wao 'muhimu' wa kikosi cha kwanza kiliwafanya waondoke kwenye ushindani na kuanza kujenga kikosi kipya.**

"Makosa tuliyofanya msimu huu ni kusajili wachezaji wengi wapya, na kocha kuanza na kikosi kipya lakini pia wachezaji wakiwa wamezoeana na kocha Juma Mwambusi kujiuzulu," alisema Kimbe.

Aliongeza mazingira ya timu kufanya vibaya iliwasababishia kubadilisha makocha uamuzi ambao kila mmoja alikuja kufundisha mfumo wake.

"Tumegundua makosa yetu, tunaimani msimu ujao hayatajirudia, tutakuwa makini katika usajili wa wachezaji pamoja na kuhakikisha tunaendelea kubaki na kocha wetu," Kimbe alisema.

"Katika Usajili tunaangalia mahitaji ya timu yetu, kama kutakuwa na uhitaji wa wachezaji wakigeni tutafanya hivyo, lakini hatuwezi kusema tutasajili nyota wa kimataifa au la," alisema Kimbe.

Hadi ligi inasimama, Mbeya City yenye pointi 30, iko katika nafasi ya 17 ikifuatiwa na Alliance FC yenye pointi 29, Mbao FC yenye alama 23 na Singida United wenye pointi 15 wakiburuza mkia.



Kocha wa Chelsea, Frank Lampard (kulia), akitoa maelekezo kwa wachezaji wake kwa ajili ya kujiweka tayari na mechi za Ligi Kuu England inayotarajiwa kurejea hivi karibuni. **PICHA : MAIL**

# *Waamuzi Zanzibar waisubiri serikali*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAAMUZI wanaochezesha Ligi Kuu Zanzibar wamesema wanaendelea kufanya mazoezi kwa lengo la kujiweka tayari kuendelea na msimu wa 2019/20, lakini wakisubiri uamuzi utakaotolewa na serikali kuhusiana na hatima ya ligi hiyo, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Kamati ya Waamuzi visiwani hapa, Muhsini Kamara, aliliambia gazeti hili waamuzi wote wanaendelea na mazoezi binafsi lakini wakitumia programu za mafunzo kupitia mitandao.

Kamara alisema waamuzi wake wanafuata pia programu zilizotolewa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), katika kipindi hiki cha corona, hivyo wanaamini hakuna kitakachoharibika.

Alisema kuwa ni vema waamuzi wote wakatekeleza programu hizo za mazoezi ambazo pia zinakumbusha sheria za soka ili kuwasahihisha sehemu zenye makosa na baadaye kurejea uwanjani wakiwa na uelewa zaidi.

Aliongeza mbali na kujikumbusha sheria za mchezo huo, lakini waamuzi wao wanafanya mazoezi ya utimamu wa mwili kwa lengo la kujiweka tayari kuanza kibarua hicho cha kuchezesha pale serikali itakapotoa baraka za kuendelea na ligi.

"Ni kawaida kwa waamuzi kuwa ni watu wenye mazoezi, hivyo waamuzi wote wanajua umuhimu wa kufanya mazoezi na kuzisoma mara kwa mara sheria 17 za soka ili kuzipatia ufumbuzi kwa zile zinazowasumbua, hata kama ligi itarudi uwanjani sisi tupo tayari kuendelea na kazi," alisema Kamara.

Kiongozi huyo ambaye ni Kamisaa anayetambulika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), amewakumbusha waamuzi wote kuendelea kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Michezo

Alhamisi Mei 21, 2020

Nipashe




Rose ampeleka Pochettino United UKURASA 22



Mshambuliaji wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mtanzania Thomas Ulimwengu, akifanya mazoezi binafsi nyumbani kwake jijini Lubumbashi ili kujiandaa na Ligi Kuu nchini humo hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

# UTAJIRI WAANZA KUNUKIA YANGA

## ●●● Wanachama waambiwa wataendelea kuimiliki klabu licha ya mfumo wa uendeshaji...

**Na Somoe Ng'itu**

MABADILIKO ya mfumo wa uendeshaji yanayotarajiwa kufanyika ndani ya Yanga hivi karibuni yanatajwa yataiongezea thamani klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

**Mchakato rasmi wa mabadiliko ya mfumo huo yalitangazwa kufanyika kuanzia juzi na utasimamiwa na wadhamini wa klabu hiyo, Kampuni ya GSM.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wanatakiwa kutokuwa na hofu ya aina yoyote kwa sababu mabadiliko hayo yatafanyika kwa weledi chini ya mwanasheria mzoefu, Alex Mgongolwa.

Nugaz alisema viongozi wa klabu hiyo wamedhamiria kuipeleka Yanga kwenye mabadiliko ambayo yatasaidia uendeshaji kuwa wa kisasa.

Alisema kila jambo lina mwanzo na kuanza kwa mchakato huu wa mabadiliko, kutaifanya Yanga kuwa moja ya timu zitakazojiendesha kisasa na kupata mafanikio yaliyokuwa yakisubiriwa kwa muda mrefu.

"Moja ya azma na sera yake (Mwenyekiti Mshindo Msolla ni kuipeleka Yanga kwenye mabadiliko, kutoka kwenye uendeshaji wa zamani na kwenda kwenye uendeshaji wa kisasa," alisema Nugaz.

Kiongozi huyo aliwataka wanachama wa Yanga kutoa ushirikiano ili mchakato huo ambao ulikwama mara kadhaa miaka ya nyuma ukamilike kwa wakati.

"GSM imekaa sawa, imelivalia njuga suala hili kwenda kwenye mabadiliko, hamu yetu wana Yanga, azma yetu wana Yanga ni kumpa ushirikiano mwenyekiti, kikubwa zaidi ni uzoefu aliokuwa nao huyu mshauri kwa kuongoza timu 42 huko Hispania, tukiungana pamoja, tutakwenda kwenye mabadiliko," alisema Nugaz.

Endapo Yanga itafanikiwa kubadili mfumo wao wa uendeshaji, itakuwa imewafuata watani zao Simba ambayo tayari walishabariki mabadiliko hayo kwenye mkutano mkuu wa wanachama uliofanyika mwaka 2018.

Katika mchakato huo, Yanga imepanga kutumia kauli isemayo "Twenzetu Kwenye Mabadiliko".

Wakati huo huo Nugaz amesema uongozi umeshajipanga kuwaandalia taratibu za usafiri makocha wake mara mipaka ya anga itakapofunguliwa huko walipo.

Baada ya Ligi Kuu Bara kusimama ili kupisha maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael na msaidizi wake walikwenda Afrika Kusini kwa ajili ya mapumziko.

# Kagere kubadili mfumo Simba

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam huenda wakalazimika kubadilisha mfumo wa kucheza katika kikosi chake kama mshambuliaji wake kinara, Meddie Kagere atachelewa kuungana na wenzake wakati ligi hiyo itakaporejea tena.

Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na ligi nyingine ikiwamo mashindano ya Kombe la FA yanatarajiwa kurejea tena hivi karibuni baada ya Rais John Pombe Magufuli kufiria kurejesha michezo nchini.

Mbali na Kagere ambaye alirejea kwao Rwanda, wachezaji wengine wa Simba ambao hawako nchini ni pamoja na Clatous Chama, Francis Kahata na Sharaf Shiboub.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema benchi la ufundi la timu hiyo litapanga mfumo kwa kuzingatia wachezaji ambao watakuwa wako tayari kwenye kikosi.

Matola alisema ni mapema kuweka wazi aina ya mfumo utakaotumika mpaka pale wachezaji wao wote watakaporipoti kambini baada ya ruhusa ya kufanya mazoezi pamoja itakapotolewa.

"Tusubiri wachezaji wote warudi kwanza, baada ya hapo ndio tutaangalia nani yupo na nani hayupo, Kocha Mkuu, Sven Vandanbroeck ataweza kubadili mfumo kwa kuangalia wachezaji tuliokuwa nao kwa kipindi hicho," alisema Matola.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wanaendelea na mazoezi kwa sababu wanataka kuona wanamalizika vizuri msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tuko tayari, tunawasubiri nyota wetu warejee, hapa kilichobakia ni kusubiri tamko rasmi la TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), ambayo itapokea rasmi ruhusa kutoka katika mamlaka husika juu za nchi," alisema Matola.

Aliongeza pia Simba iko tayari kupokea uamuzi utakaochukuliwa na shirikisho hilo kuhusu mtindo utakaotumika kumalizia ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), Kagere ndio kinara wa kupachika mabao akiwa amefunga mabao 19.

Simba yenye pointi 71, imebakiza michezo 10 ili imalize msimu na tayari imesharudiana na wapinzani wake kwenye vita ya ubingwa ambao ni Yanga na Azam FC.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >